

UCHANGANUZI WA KIRAI CHA KIBANTU – MTAZAMO WA X-BAA

MFANO: KUTOKA KIRAI NOMINO NA KIRAI KITENZI CHA

KINYAKYUSA

MARY NATHANIEL KANICHI

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA

MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI

YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2018

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma kazi hii na hapa anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kikubali kupokea tasnifu hii: *Uchanganuzi wa Kirai cha Kibantu – Mtazamo wa X-baa mfano: Kutoka Kirai Nomino na Kirai Kitenzi cha Kinyakyusa* katika kukamilisha masharti ya shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dr. Hanna Simpassa

(Msimamizi)

Tarehe _____

HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, au kutoa tasnifu hii kwa njia yoyote ile Kielektroniki, Kurudufu nakala, Kurikodi bila ya idhini ya mwandishi au idhini ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

TAMKO

Mimi, **Mary Nathaniel Kanichi**, nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote.

Sahihi

Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mme wangu Bwana Johnson Nasson Katabwa pamoja na familia yangu ya Bwana Nathaniel Kanichi, ndugu zangu Andrew, Magreth , Olban na binamu zangu Agatha Kachamila na Helen Kachamila, Mchungaji Prosper na Debora Ntepa ambao wakati wote walinisaidia kila nilipohitaji msaada na kuniombea. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awabariki na awajaze vile vyote walivyopoteza kwa ajili yangu.

SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati kwa Mwenyenzi Mungu, Mfalme wa Utukufu, ambaye amekuwa chanzo cha nguvu na mafaniko yangu. Bila yeye nisingefika popote katika kazi hii. Natoa shukrani zangu kwa mme wangu Johnson Nasson Katabwa, mzazi wangu Bwana Nathaniel Kanichi na ndugu zangu Andrew, Magreth na Olban.

Shukrani zangu ziende kwa msimamizi wangu wa tasnifu ya Shahada ya Uzamili Dr. Simpassa Hanna kwa msaada wake, hasa kwa kuikosea kazi yangu pale nilipokosea, pia kwa kunipa msaada wa kuniielekeza pale nilipokwama katika kuelewa kufanikisha kazi hii. Pia napenda kuwashukuru Wachungaji Zephrene Kahingwa wa Kanisa la TAG Chato mjini, Mchungaji Bigirwa wa Kanisha la TAG Karangwe Chanika na Mama Mchungaji Praxidia Kahigwa kwa kuniombea na kunitia moyo.

Shukrani pia kwa Bw na Bi. David Mwakyusa, Julius Mwaipopo, sifa Mapamba, Hilda Mwakyilete wa Ipinda Kyela na wote walioshiriki katika kunipa data zote kuhusiana na utafiti wangu, ambazo zimetumika katika kazi hii.

Shukrani pia ziende kwa Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI) katika maktaba ndogo ya Makavazi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa msaada wao wa kunipa nafasi hii kusoma katika Maktaba.

Shukrani zangu pia ni kwa mkuu wangu wa kituo cha kazi Shule ya Sekondari Chato Mwalimu Selema Majura Bernado, Afisa Elimu Sekondari Bw. Joackim Njiani,

Bahati Onesmo Afisa Elimu Takwimu Halmashauri ya Chato, wanafunzi wenzangu Leticia, na Luzinga ambao walinisaidia hata nikaweza kukamilisha kazi hii. Naomba Mungu awape nguvu katika kila wanalolifanya.

IKISIRI

Uchanganuzi wa Kirai Nomino na Kirai Kitenzi cha Kinyakyusa ni mada ambayo iliyofanyika kwa kushirikisha watafitiwa 10 wazawa wa lugha hiyo wakiwemo walimu na wanafunzi wenye ufahamu wa dhana ya virai. Wazee watano (5), vijana watatu (3) na watoto wawili (2) kutoka katika kijiji cha Ipinda, kata ya Ipinda wilaya Kyela, mkoa wa Mbeya walishirikishwa. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza na kuchanganua virai vya kibantu mfano kutoka katika kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Virai hivi vya Kinyakyusa vimeweza kubainishwa na kuonyesha vinavyojitokeza katika lugha hiyo. Pia virai hivyo vimeainishwa kwa kuzingatia miundo yake na kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Imeonekana kuwa nadharia ya hii ya X-baa inautoshelevu wa kuweza kuchanganua, kufafanua na kuelezea virai vya lugha nyingi za kibantu, mfano kutoka katika virai hivi vya Kinyakyusa. Nadharia hii inaelezea kuhusu uwili kuwa kifundo hugawika katika matawi mawili pekee hivi ni kusema kuwa KN hakiwezi kuzalisha matawi matatu. Maelezo haya yametumika katika kuchanganua virai hivi vya Kinyakyusa. Virai vimeweza kubainishwa kwa kuonyeshwa vinavyojitokeza katika lugha hiyo, kuainishwa kwa kuzingatia miundo yake na pia kuchanganuliwa kikamilifu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa. Matokeo ya utafiti huu yamegusia tu uchanganuzi wa virai viwili yaani kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa. Hivyo utafiti ufanyike zaidi katika uchanganuzi wa virai vingine na tungo ambazo utafiti huu haukushughulikia katika lugha hii ya Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	ii
HAKI MILIKI.....	iii
TAMKO	iv
TABARUKU.....	v
SHUKRANI.....	vi
IKISIRI	viii
JEDWALI.....	xiii
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI	1
1.1 Utangulizi wa Sura ya Kwanza	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti	1
1.3 Historia Fupi Kuhusu Nadharia ya X-baa	2
1.3.1 Historia fupi ya Jamii ya Wanyakyusa.....	3
1.4 Tatizo la Utafiti	4
1.5 Malengo ya Utafiti	5
1.5.1 Lengo Kuu.....	5
1.5.2 Malengo Mahususi	5
1.6 Maswali ya Utafiti.....	6
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.8 Mawanda ya Utafiti	7
1.9 Mipaka ya Utafiti	7
1.10 Hitimisho.....	8

SURA YA PILI.....	9
2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA	9
2.1 Utangulizi wa Sura ya Pili.....	9
2.2 Dhana ya X-baa na Kirai	9
2.2.1 Dhana ya X-baa.....	9
2.2.2 Dhana ya Kirai	11
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Uchanganuzi wa Sentensi.....	14
2.4 Kiunzi cha Nadharia.....	16
2.4.1 Nadharia ya X-baa.....	16
2.5 Hitimisho.....	18
SURA YA TATU	19
3.0 MBINU ZA UTAFITI.....	19
3.1 Utangulizi	19
3.2 Eneo la Utafiti	19
3.3 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	19
3.3.1 Mbinu ya Usaili	20
3.3.2 Mbinu ya Ushiriki	21
3.4 Vifaa vya Utafiti.....	22
3.5 Sampuli na Usampulishaji.....	22
3.5.1 Sampuli.....	22
3.5.2 Usampulishaji.....	23
3.6 Mkabala wa Utafiti.....	24
3.7 Maadili ya Utafiti	25
3.8 Changamoto Zilikazojitokeza Wakati wa Ukusanyaji Data	25

3.9	Hitimisho	26
SURA YA NNE.....		27
4.0	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA	
	DATA.....	27
4.1	Utangulizi	27
4.2	Kubainisha Virai vya Kinyakyusa.....	27
4.3	Kuainisha Virai vya Kinyakyusa kwa Kuzingatia Miundo Yake	29
4.3.1	Kirai Nomino (KN)	29
4.3.2	Kirai Kitenzi (KT).....	36
4.3.3	Kirai Vumishi (KV)	45
4.3.4	Kirai Kielezi (KE)	47
4.3.5	Kirai Kihusishi (KH).....	49
4.4	Kuchanganua Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT) vya Kinyakyusa - Mtazamo wa X-baa	53
4.4.1	Kirai Nomino.....	55
4.4.2	Kirai Kitenzi (T).....	66
4.5	Hitimisho.....	84
SURA YA TANO		85
5.0	MATOKEO YA UTAFITI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO	85
5.1	Utangulizi	85
5.2	Muhtasari wa Utafiti.....	85
5.3	Matokeo ya Utafiti	86
5.4	Mchango wa Utafiti.....	86
5.5	Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo	87

5.6	Hitimisho	88
	MAREJEO.....	89
	VIAMBATANISHO.....	92

JEDWALI

Jedwali 3.1: Idadi ya Watafitiwa kwa Kuzingatia Umri na Kiwango cha Elimu 24

ORODHA YA VIFUPISHO

KN	Kirai Nomino
KT	Kirai Kitenzi
KV	Kirai Kivumishi
KH	Kirai Kihusishi
KE	Kirai Kielezi
Kij	Kijalizi
Kib	Kibainishi
Ktg	Kishazi tegemezi
X'	Kagoria za maneno (N', T', V', E' na H')
S	\bar{K} ishazi kijalizi
N	Nomino
T	Kitenzi
W	Kiwakilishi
V	Kivumishi
E	Kielezi
H	Kihusishi

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi wa Sura ya Kwanza

Utafiti huu unahusu Uchanganuzi wa Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT) cha Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Mtafiti ameshughulika katika kubainisha virai vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa, kuainisha virai hivyo kwa kuzingatia miundo yake na kuchanganua virai viwili yaani kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Sura hii ya Kwanza imegawanyika katika sehemu tisa (9). Sehemu ya kwanza imeanza kwa kutambulisha mada ya utafiti, Sehemu ya Pili inaelezea usuli wa tatizo, historia ya nadharia ya X-baa na historia fupi ya jamii ya Wanyakyusa. Sehemu ya tatu inaeleza tatizo la utafiti. Sehemu ya nne inaeleza malengo ya utafiti kwa kuangalia lengo kuu na malengo mahususi. Sehemu ya tano maswali ya utafiti yaliyomsaidia mtafiti kumpa mwelekeo wa utafiti wake. Sehemu ya sita inaeleza umuhimu wa utafiti katika jamii, elimu, na kwa watafiti wengine. Sehemu ya saba mawanda ya utafiti. Sehemu ya nane mipaka ya utafiti na sehemu ya tisa hitimisho la Sura hii ya Kwanza.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tafiti nyingi zimefanyika kuhusu uchanganuzi wa sentensi, vishazi, kirai nomino na kijalizo kwa kutumia nadharia ya X-baa. Mfano Jerom (2008) na Nyaga (2011) walitafiti kuhusu vishazi huru vya Kiswahili vinavyoweza kuchanganuliwa kwa

kutumia nadharia ya X-baa. Aidha, watafiti wengine mfano Koech (2013) alichunguza kijalizo cha Kiswahili kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya X-baa na Olali (1997) alitafiti kuhusu kirai cha Kiswahili kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya X-baa. Lakini, kirai cha Kinyakyusa hakijashughulikiwa kabisa katika mtazamo huu wa X-baa. Lusekelo (2009) yeye amejaribu kuchunguza kirai nomino cha Kinyakyusa kwa kujikita zaidi katika kuchanganua vipengele vinavyounda kirai hicho, lakini hakutumia nadharia ya X-baa. Hivyo utafiti huu uliona ipo haja ya kuziba pengo na kupiga hatua ya kuchanganua virai vya lugha nyingine za kibantu na mfano kutoka katika kirai cha Kinyakyusa.

1.3 Historia Fupi Kuhusu Nadharia ya X-baa

Nadharia ya X-baa iliasisiwa na Jackendoff na kuendelezwa na Chomsky katika jaribio la kuonyesha miundo ya virai vya lugha. Pamoja na nadharia hii Chomsky pia aliunda Nadharia ya Sarufi Bia ambayo utumika kuchanganua lugha mbalimbali ikijikita katika ufuataji sheria au kanuni zinazohusika katika uundaji wa maneno. Nadharia ya X-baa inatumika kuelezea miundo ya virai vya kila lugha, ni miongoni mwa nadharia zinazouundwa na nadharia ya Sarufi Bia.

Nadharia hii ilitokana na upungufu ulioonekana kuwepo katika nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Cowper (1992), anasema kuwa nadharia ya X-baa ilitolewa ili kufidia upungufu wa nadharia ya kanuni muundo virai ambayo ilihitaji kuthibitiwa. Anaeleza kuwa nadharia ya kanuni muundo virai haikutambua uhusiano wa karibu kati ya kichwa na kijalizo chake. Anafafanua kuhusu uteuzi, yaani uwezo wa

kategoria leksika kuchagua kijalizo katika tungo. Hivyo nadharia ya X-baa ilizuka kama suluhisho la upungufu huu kama asemavyo Newmeyer (1986), nadharia ya X-baa ilibadilisha kanuni za miundo virai kwa kutumia ishara hizi:

X" [kibaimshi cha X'] X'

X'-----► X...

Kwa kufanya hivi kategoria zote zimekuja kuwakilishwa kwa ishara moja hivyo kuondolea mbali umuhimu wa kategoria. Aidha kinyume na nadharia ya Sarufi Miundo Virai nadharia hii inaonyesha mahusiano ya ndani baina ya neno kuu (kichwa) na maneno au mafungu ya maneno mengine. Haegeman (1994) anadai kuwa kulingana na nadharia hii virai vyote vinatawaliwa na neno kuu yaani X. maneno hayo makuu ni vitengo vya chini kabisa na hutawala maneno mengine.

1.3.1 Historia fupi ya Jamii ya Wanyakyusa

Wataalamu mbalimbali wamejaribu kuelezea historia ya Wanyakyusa, mfano Mekacha (2000) anasema, Lugha ya Kinyakyusa ni miongoni mwa lugha za kibantu inayozungumzwa nyanda za juu Kusini mwa Tanzania bara katika mkoa wa Mbeya. Katika mgawanyo wa lugha za kibantu, Kinyakyusa kimewekwa katika kundi la M.30 na kupewa msimbo wa M.31 (taz. Guthrie, 1948; Mabo, 1999 na Mabo na Sands. 2002). Guthrie (kishatajwa) uanishaji wake ulizingatia kigezo cha kijiografia kuliko kigezo cha kiisimu na hii ndiyo sababu lugha ya Kinyakyusa hutofautiana na lugha zinazopakana nayo ambazo ni Kindali, Kimalila, Kisafwa na Kinyika. Lugha ya Kinyakyusa nayo haina mwingiliano mkubwa wa kiisimu na lugha hizo kama ilivyo katika Kiswahili. Felberg (1990) Wazungumzaji wazawa wa lugha ya

Kinyakyusa wanapatikana zaidi katika wilaya ya Rungwe na Kyela katika mkoa huo wa Mbeya ingawa pia Kinyakyusa kinazungumzwa Kaskazini mwa mto Rukuru nchini Malawi. Kinyakyusa kinakadiriwa kuwa na wazungumji zaidi ya milioni moja. Wikipedia (2013) Wanyakyusa wapo wa aina mbili nao ni Wanyakyusa wa Tukuyu na Wanyakyusa wa Kyela wanaozungumza lugha moja ya Kinyakyusa ambayo hapo awali walijulikana kama wakonde. Kutokana na maelezo ya watafiti hao inaonyesha kuwa lugha hii ya Kinyakyusa haina lahaja nyingi. Historia hii fupi ya jamii ya Wanyakyusa imemsaidia mtafiti katika kuchagua eneo moja la utafiti wilaya ya Kyela katika kijiji cha Ipinda eneo mbalo mtafiti anauzoefu nalo ili kuchunguza kirai cha lugha hii ya Kinyakyusa,

1.4 Tatizo la Utafiti

Nadharia ya X-baa inaonekana kupiga hatua kubwa sana katika jitihada za wanaisimu za kuunda sarufi bia inayoweza kutumika kuchambua lugha mbalimbali za wanadamu duniani (www.academic.edu 2014). Moja ya vigezo vinavyoangaliwa katika kutathmini kufaa kwa nadharia mbalimbali ni kuona kama nadharia hiyo ina utoshelevu wa kiufafanuzi, uchanganuzi na kiuelezaji (Chomsky, 1957). Kwa mantiki hiyo watafiti wengi wametumia nadharia ya X-baa wakijaribu kuonyesha utoshelevu wake katika kuchambua virai vya lugha ya Kiswahili, vishazi huru vya lugha Kiswahili na vijalizo vya lugha ya Kiswahili. Mfano Jerom (2008) na Nyaga (2011) walitafiti kuhusu vishazi huru vya Kiswahili vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Aidha. watafiti wengine mfano Koech (2013) alichunguza kijalizo cha Kiswahili kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya X-baa na Olali (1997) alitafiti kuhusu kirai cha Kiswahili

kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya X-baa. Hivyo basi, lengo la utafiti huu ni kutaka kuona kama nadharia hii ina utoshelevu wa kiuchanganuzi, kiufafanuzi na kuelezeji wa virai vya lugha ya Kinayakyusa kwa sababu kila lugha ina tofautiana na nyingine katika mipangilio ya maneno katika kuunda virai nomino na vitenzi. Mfano Katika Kiingereza, kivumishi huja kabla ya neno kuu “My father built a big house” wakati katika Kiswahili Kivumishi huja baada ya neno kuu “baba yetu alijenga nyumba kubwa” katika Kinyakyusa kivumishi huja baada ya neno kuu mfano “ Tata gwitu ajengile inyumba inywamu” Hivyo mtafiti alikusudia kuona kama nadharia hii ina utoshelevu wa kiuchanganuzi, ufafanuzi na uelezaji wa virai nomino na virai tenzi vya Kinyakyusa.

1.5 Malengo ya Utafiti

Adam (2008) anaeleza kuwa malengo ya utafiti ni yale malengo yaliyokusudiwa na mtafiti. Malengo hutueleza mtafiti anataka kupata nini mwisho wa utafiti wake. Utafiti una malengo natatu, lengo kuu na malengo mahususi mawili.

1.5.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza Virai nomino na virai tenzi vya lugha ya Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa ili kuona kama nadharia hii ina utoshelevu wa kuichanganuzi na kielezaji.

1.5.2 Malengo Mahususi

- i) Kubainisha muundo virai nomino na virai tenzi vya Kinyakyusa.
- ii) Kuchanganua virai nomino na virai tenzi vya Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa

- iii) Kuelezea ufaafu wa nadhari ya X-baa katika kuchanganua kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa.

1.6 Maswali ya Utafiti

- i) Je, virai nomino na virai tenzi vya lugha ya Kinyakyusa vina muundo gani?
- ii) Je, virai nomino na virai tenzi vya Lugha ya Kinyakyusa vinaweza kuchanganuliwa kikamilifu kwa kutumia nadharia ya X-baa?
- iii) Je, Nadharia ya X- baa ina inafaa katika kuchanganua Kirai nomino (KN) na Kirai tenzi (KT) cha lugha ya Kinyakyusa?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umekusudia kutoa mchango mkubwa katika taaluma ya Sintaksia ya uchanganuzi wa virai, kwa kujikita zaidi katika uchanganuzi wa virai nomino (KN) na virai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Ni dhahiri kwamba utafiti huu atatoa mchango wa kutosha kwa wanaisimu kuhusiana na uchanganuzi wa virai vya lugha nyingine za Kibantu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa, na hivyo kuweza kufahamika kwa watu wengine wasio na uzoefu na nadharia hii.

Kwa namna nyingine utafiti huu utasaidia na kutumika kama zana ya kufundishia sintaksia ya uchanganuzi wa virai katika mtazamo wa X-baa vyuoni na vyo vikiu hususani katika lugha nyingine za kibantu ambazo hazijashughulikiwa kabisa kwa mtazamo huu wa X-baa. Hivyo ni kazi itakayotoa dira na mwelekeo kwa vizazi vya wasomi vijavyo. Pamoja na hayo, utafiti huu utakuwa ni changamoto kwa

wanafunzi wa sintaksia kupenda kujifunza na kuelewa michakato iliofanyika katika kupunguza au kuondoa sheria nyingi zilizotumika katika taaluma hii ya uchanganuzi wa lugha za Kibantu.

Matokeo ya kazi hii yatawasaidia wataalamu mbalimbali wanaofanya tafiti kuhusu uchanganuzi wa virai, vishazi na sentensi za lugha za Kibantu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa katika makabila mbalimbali. Hivyo utafiti huu ni mwanzo utakaotazamiwa kutoa changamoto ya kuendeleza kufanya tafiti zaidi kuhusiana na uchanganuzi wa kirai, kishazi na sentensi kwa kutumia nadharia ya hii ya X-baa.

Vile vile utafiti huu utachangia maarifa mapya katika taaluma ya sarufi miundo kwa kuelewa jinsi tungo virai vya lugha nyingine za kibantu zinavyoweza kuchanganuliwa kwa mtazamo wa X-baa.

1.8 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu luulijikita katika kubainisha muundo ya kirai nonimo na kirai tenzi cha Kinyakyusa, kuainisha virai hivyo kwa kuzingatia muundo wake na kuvichanganua kwa kutumia nadharia ya X-baa. Utafiti haukuhusisha viwango vingine vya tungo kama vile kishazi huru cha Kinyakyusa, kijalizo, uchanganuzi wa sentensi na uchanganuzi wa kirai elezi, kivumishi na kihusishi vya lugha hii ya Kinyakyusa kwa sababu ya upana kwa mada hii. Aidha utafiti huu ulihushisha kijiji cha Ipinda kilichopo katika wilaya ya Kyela mkoani Kyela eneo ambalo mtafiti ana uzoefu nalo.

1.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kubainisha aina za virai vya Kinyakyusa, kuchanganua virai kwa kutumia nadharia ya X-baa, na kutumia nadharia hii kuelezea ufaafu wake

katika kuchanganua virai viwili yaani kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) vya lugha ya Kinyakyusa. Kijiji kilichoshirikishwa katika utafiti huu ni Ipinda kilichoko katika kata ya Ipinda wilaya ya Kyela eneo ambalo mtafiti ana uzoefu nalo na aliwahi kuishi katika wilaya hiyo ya Kyela mkoa wa Mbeya.

1.10 Hitimisho

Katika sura hii vipengele vilivyofafanuliwa ni utangulizi, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Aidha, mawanda ya utafiti na mipaka. Usuli wa tatizo umemsaidia mtafiti katika kuchunguza tatizo la utafiti. Pia mtafiti ameyatumia malengo ya utafiti katika kujibu maswali ya utafiti.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA

2.1 Utangulizi wa Sura ya Pili

Lengo la sehemu hii ya mapitio ya vitabu ni kuangalia yale ambayo wataalamu mbalimbali wamezungumzia kuhusu mada ya utafiti. Katika sehemu hii mtafiti ameangalia dhana ya X-baa, dhana ya Kirai kwa ujumla na Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu uchanganuzi wa sentensi, Kiunzi cha nadharia na amemaliza kwa hitimisho.

2.2 Dhana ya X-baa na Kirai

Waandishi mbalimbali wamejaribu kuzungumzia kwa kutoa mawazo yao kuhusu nadharia ya X-baa na dhana hii ya virai kama ifuatavyo:

2.2.1 Dhana ya X-baa

Radford (1988) ameleza kuhusu nadharia ya X-baa anasema kuwa, nadharia ya X-baa inazingatia ugawaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi. Ni upangaji unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki kipi.

Haegeman (1991) katika kuelezea nadharia ya X-baa, ameeleza kuhusu uchanganuzi wa virai kwa kuzingatia kategoria na vile vile uchanganuzi wa vishazi. Anasema kuwa katika nadharia ya X-baa kila kirai humilikiwa na kichwa leksika. Maelezo ya mtaalamu huyu yamemsaidia mtafiti katika utafiti wake kubaini aina za virai hususani pale anaposema “kila kirai humilikiwa na kichwa leksika”.

Massamba (2004) anasema, nadharia ya X-baa ni nadharia ya sarufi miundo iliyoendelezwa baada ya ile ya sarufi miundo virai. Hoja muhimu katika nadharia hii ni kwamba sheria za sarufi miundo virai hazina budi kuthibitiwa; na kwamba kategoria zaidi za virai hazina budi kuongezwa kwa mfano katika kategoria ya virai nomino kuna haja ya kuingiza kategoria nyingine ambazo ni kubwa kuliko nomino lakini ndogo kuliko kirai.

Radford (2004) anaeleza kuhusu uwili wa nadharia ya X-baa. Maelezo yake ni muhimu anasema kuwa kifundo hugawika katika matawi mawili pekee hivi ni kusema kuwa KN hakiwezi kuzalisha matawi matatu. Maelezo yake ni muhimu katika utafiti huu, kwa sababu utafiti huu umetumia kielelezo cha matawi kuchanganua kirai cha Kinyakyusa.

Radford (1988) anasema, nadharia ya X-baa hutumia alama saidizi ya X, ya taratimu (X') na X'', alitumia alama saidizi ya X' na Chomsky alitumia alama saidizi ya X. aandishi wengine hutumia alama hizi kwa mfano Jackendaff (1977) anatumia alama saidizi ya X katika anwani (it is called X syntax) lakini katika kitabu kizima anatumia alama X'.

Jackendoff (1977) akinukuliwa na Radford (1988) alitoa kanuni ya miundo virai ambayo ni

$$X^n \longrightarrow \dots X^{n-1}$$

Neno kuu katika kirai chochote linajulikana kama X'' na kategoria kirai inayobeba X' inajulikana kama X'' au X-baa mbili na kategoria inayobeba X' ni \bar{X} au X-baa moja. X ni kategoria za maneno kama vile N, V, T, E na H. Xⁿ inawakilisha X, X au

X na alama za dukukudu zinawakilisha viambajengo vinavyoweza kuongezwa. Alama zilizobainishwa hapo juu zimesaidia katika utafiti huu kuchanganua kirai cha Kinyakyusa kwa kubainisha neno kuu (kichwa) na uhusiano wake na maneno mengine yanayoambatana nalo.

Cowper (1992), anasema kuwa nadharia ya X-baa ilitolewa ili kufidia upungufu wa nadharia ya kanuni muundo virai ambayo ilihitaji kuthibitiwa. Anaeleza kuwa nadharia ya kanuni muundo virai haikutambua uhusiano wa karibu kati ya kichwa na kijalizo chake. Anafafanua kuhusu uteuzi, yaani uwezo wa kategoria leksika kuchagua kijalizo katika tungo.

Radford (1988), amefafanua virai tofauti akitumia nadharia ya X-baa katika lugha ya Kiingereza. Kazi hii ni muhimu katika utafiti huu, kwa sababu utafiti umehusu ubainishaji, uainishaji na uchanganuzi wa virai vinavyofafanua neno kuu katika kirai husika tukiitumia nadharia ya X-baa.

2.2.2 Dhana ya Kirai

Kirai ni neno au fungu la maneno linalodokeza maana lakini maana hiyo si kamilifu. Haina muundo wa kiima – kiarifu kama ule wa sentensi bali kinabeba tu sehemu ya sentensi. Kamusi ya Longhorn (2011), inadai kuwa kirai ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima – kiarifu. Massamba (2004:35), anadai kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima – kiarifu (yaani hakihusishi mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa.)

Masebo (2007) anasema, kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja na kuendelea lakini ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu. Muundo wa kiima na kiarifu ni ule ambao unadhihisha mtendaji wa tendo au tendo linalotendwa na ambalo ndiyo muundo wa msingi katika lunga yoyote ile. Anaendelea kusema kuwa katika kirai miundo ya tungo huhusisha neno moja au zaidi ambayo huwekwa pamoja katika mpangilio maalumu unaozingatia uhusian uliopo baina ya neno kuu na maneno mengine. Kwa mfano uhusiano uliopo kati ya nomino na maneno yanayoambatana nayo hutupa kirai nomino:

- **mtoto** yule
- **mtoto** yule mzuri kuliko wote
- **mtoto** yule mjinga
- **mwalimu** hodari

Katika mifano hiyo neno kuu ni **mtoto** na **mwalimu** ambazo ni nomino. Hii ina maana kwamba katika tungo hizi, nomino ndio chimbuko la uhusiano uliopo katika maneno yote yanayohusika katika kila kirai. Kwa maana nyingine tunaweza kusema tungo hizi ni *virai nomino*. Mtaalamu huyu ameendelea mbele zaidi pale anapotaja “miundo ya kirai inaozingatia mpangilio maalumu ya uhusiano baina ya neno kuu na maneno mengine” Maelezo yake yamesaidia katika ubainishaji na uanishaji wa miundo ya kirai cha Kinyakyusa.

Culicover (1976:11), anadai kuwa kirai ni mfuatano wowote wa maneno katika lugha yoyote na maneno yenyewe ni ya kategoria fulani. Kuna mfuatano wa maneno ulio mfupi kuliko sentensi lakini ni ndefu kuliko neno moja. Kwa hiyo, kuna virai

vilivyo virefu kuliko neno moja lakini fupi kuliko sentensi. Anaendelea kudai kuwa, sentensi pia ni ya kategoria fulani ya kirai kinachoitwa sentensi. Kirai pia kinaweza kuwa neno moja. Kwa mfano: *Laileti* ni mrembo.

Laileti ni kirai nomino ijapokuwa kimeundwa kwa neno moja.

Radford (2004:14), anadai kuwa kila kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai chote. Kwa mfano: *Mwanafunzi* wa Hisabati.

Mwanafunzi (umoja) ni kichwa cha kirai na ndicho kinachoamua sifa za kirai husika. Kirai huainishwa kimuundo kulingana na neno kuu/ kichwa cha kirai husika. Kwa mfano: Kirai ambacho neno lake kuu ni nomino/ au kiwakilishi huitwa kirai nomino, kwa mfano: *Mtoto huyu*. Hapa neno kuu ni mtoto, ndipo kirai hicho kikaitwa kirai nomino. Kirai kinaelezwa kuwa ni tungo ambayo haihusishi kitendo na yule anayetekeleza. Uainishaji wa virai kimuundo hutegemea neno kuu katika kirai hicho. Kwa kufuata mkabala huu tuna aina zifuatazo za virai: virai nomino, virai vivumishi/virai vumishi, virai vielezi/virai elezi, virai vitenzi/virai tenzi, virai vihusishi/virai husishi. Maelezo haya yametumika katika ubainishaji na uainishaji wa aina za virai vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa kwa kuzingatia muundo wake.

Matei (2008) kirai ni fungu la maneno ambalo hufanya kazi kama neno moja au huwa na uamilifu sawa. Hivyo kirai ni fungu la maneno ambalo huundwa na neno moja au zaidi. Maelezo haya yamesaidia katika kubaini kirai cha Kinyakyusa

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Uchanganuzi wa Sentensi

Kazi tangulizi ni kazi ambazo tayari zimefanywa na watafiti wengine waliotangulia kuhusu mada ya utafiti ama inayokaribiana na mada husika. Ni kazi zinazotoa dira katika kubaini pengo la utafiti na kutoa mwelekeo katika tafiti nyingine. Kwa kupitia kazi mbalimbali za watafiti, mtafiti ameweza kubaini pengo la utafiti kwa kusoma kazi za watafiti wengine mfano; Lusekelo (2009) aliyeangalia muundo wa kirai nomino cha Kinyakyusa kwa kujikita zaidi katika uchanganuzi wa vipengele vinavyojenga kirai hicho. Mtafiti huyo hakuchunguza uwezeakano wa virai hivyo kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Hivyo basi mtafiti aliona ipo haja ya kuchunguza na kuchanganua kirai hicho kwa kutumia nadharia hii ya X-baa. Utafiti huu ulifanyika nchini Tanzania.

Elali (2012) yeye alijikita zaidi katika kuchanganua kikundi nomino cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa. Utafiti huo ulifanyika nchini Kenya-Nairobi. Alibainisha miundo ya kikundi nomino cha Kiswahili na kukichanganua kwa mtazamo wa X-baa. Utafiti huo umesaidia katika kubaini pengo la utafiti huu na kumsukuma mtafiti katika kutafiti zaidi kuhusu uchanganuzi wa virai nomino (KN) na virai tenzi vya Kinyakyusa kwa kutumia nadharia hii ya X-baa.

Mbesa (2008) akinukuliwa na Koech yeye katika utafiti wake alijikita zaidi katika kuchanganua kishazi nomino cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa. Katika kazi yake alifafanua vishazi vijalizi vya nomino na kitenzi na kuvichanganua kwa mtazamo wa X-baa. Utafiti huu umesaidia katika kuongezea data za utafiti kuhusu nadharia ya X-baa. Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya - Nairobi.

Olali (1997) naye pia katika utafiti wake alichanganua virai kwa kutumia nadharia ya X-baa kwa kuonyesha uhusiano dada. Kazi yake imesaidia katika kubaini uhusiano dada katika uchanganuzi wa virai. Ameonyesha namna ya kuchanganua XP iliyo na virai vingi ndani yake. Alionyesha namna ya kuchanganua XP ilivyo na virai vingi ndani yake. Utafiti huu pia ulifanyika nchini Kenya – Nairobi.

Koech (2013) akinukuu kazi ya Nyaga (2011) yeye alichanganua kishazi elezi cha Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya X-baa. Alijishughulisha zaidi katika kuchunguza namna nadharia ya X-baa inavyozingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti tofauti. Kazi hii imetufaa kwa sababu imetupa msingi wa nadharia ya X-baa. Anasema kuwa nadharia ya X-baa huzingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti tofauti. Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya, Nairobi.

Jerome (2008) akinukuliwa na Koech katika kazi yake, alijikita zaidi katika kuchanganua kishazi huru arifu cha Kiswahili kwa mtazamo wa X-baa. Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya - Nairobi. Alibainisha kishazi huru arifu cha Kiswahili na kukichanganua kwa kutumia nadharia hiyo ya X-baa. Utafiti wake umesaidia katika kuelewa matumizi ya nadharia ya X-baa katika uchanganuzi wa viungo vya sentensi. Anasema kuwa nadharia ya X-baa inatumika kuelezea miundo ya virai ya kila lugha na ni miongoni mwa nadharia zinazotumika kuunda nadharia ya sarufi bia.

Koech (2013) alichunguza na kuchanganua kijalizo cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa. Alibainisha uamilifu wa kijalizo katika tungo na kubainisha miundo tofauti ya vijalizo na kudhihirisha sheria zinazotawala uunganishwaji wa

vipashio vinavyojaliza virai tofauti katika sentensi. Kazi hii imesaidia katika kuongeza data katika utafiti huu. Utafiti huu pia ulifanyika nchini Kenya – Nairobi.

Hivyo basi inaonyesha kuwa tafiti nyingi zimefanyika kwa kutumia nadharia ya X-baa. Watafiti wengi waliotafiti walichunguza uchanganuzi wa kirai nomino, kishazi huru arifu, kishazi nomino kijalizi na kijalizo katika lugha ya Kiswahili, na inaonyesha kuwa utafiti wa uchanganuzi wa Kirai cha lugha nyingine za kibantu kwa kutumia nadharia ya X-baa haujafanyika bado. Tafiti zote hizi zimefanyika nchini Kenya. Nchini Tanzania, utafiti wa uchanganuzi kirai, kishazi na sentensi kwa kutumia nadharia ya X-baa inaonyesha bado haujafanyika. Hivyo kutokana na matokeo hayo ya tafiti tangulizi mtafiti ameweza kubaini pengo la utafiti na kuona kwamba ipo haja ya kufanya utafiti zaidi kwa kutumia nadharia ya X-baa kwa kuchanganua kirai cha lugha nyingine za kibantu: mfano kutoka katika kirai nomino na kirai kitenzi cha Kinyakyusa. Pia tafiti hizo zimesaidia katika kuongeza data katika utafiti huu.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia kama inavyoelezwa na Massamba (2004) ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo. Kiunzi cha nadharia ambacho kitatumika katika utafiti huu ni nadharia ya X-baa.

2.4.1 Nadharia ya X-baa

Utafiti huu umetumia nadharia ya X-baa katika kubainisha, kuainisha na kuchanganua virai nomino na virai tenzi vya lugha ya Kinyakyusa.

Nadharia hii ya X-baa iliasisiwa na Jackendoff na kuendelezwa na Chomsky katika jaribio la kuonyesha miundo ya virai vya lugha. Ilitumika katika kuonyesha na kusawazisha miundo ya virai. Nadharia hii ya X-baa iliundwa kutokana na wingi wa sheria zilizotumika katika kuonyesha miundo virai katika Sarufi ya Miundo Virai. Katika nadharia hii kuna kaida za ufasiri wa kategoria za virai kutoka kwa kategoria leksika pamoja na masharti ya mpangilio wa kidaraja wa kategoria kwa kutegemea hadhi ya vipashio vya kategoria leksika vinavyounda kirai fulani. Haegeman (1994) anadai kuwa kulingana na nadharia hii virai vyote vinatawaliwa na neno kuu. Ufasiri wa neno kuu la kirai ni sufuri yaani X. Maneno haya makuu ni vitengo vya chini kabisa na hutawala maneno mengine.

Nadharia hii vile vile inatofautisha viwango viwili vingine vya ufasiri wa “baa” moja yaani X'. Chagizo huungana na X' ili kuunda ufasiri wa kiwango cha “baa” moja yaani X'. hadhi ya juu ya kirai inapatikana kwa kuunganisha X' ya juu kabisa na kibainishi ili kuunda ufasiri wa juu kabisa wa X''.

Katika nadharia ya X-baa kichwa cha kirai kinaweza kutangualia au kuwa mwisoni mwa maneno yanayounda kirai husika. Lugha mbalimbali huweka vigezo vyake vya neno kuu (Haegeman 1991). Kinyakyusa ni lugha iliyo na neno kuu mwanzo; wakati mwingine huweza kutanguliwa na kibainishi. Japokuwa vijalizo na vibainishi ni muhimu katika ufasiri wa hali ya juu kabisa wa kirai, wakati mwingine vinaweza kutokuwepo. Katika hali hii, nafasi hii huchukuliwa kuwa kapa. Kwa mfano katika kirai hiki “kikombe changu” kategoria “kikombe” hufasiriwa kwa baa moja kuongezwa kijalizo “changu” na kufasiri zaidi kwa baa ya pili kwa kuongezwa

kibainishi “hiki” katika mfano huu neno kuu la kirai hiki ni nomino na hivyo kuwa kirai nomino. Wakati ambapo kibainishi na kijalizo havipo, kirai hupata ufasiri wa baa mbili ili kuwepo na hali ya usawazisho wa kimuundo kwani nafasi hizi zaweza kujazwa ama kuwa kapa. (Ouhalia 1991:52)

Pia nadharia hii ya X-baa inaelezea uwili wa nadharia hii katika kuchanganua kirai ambapo kifundo hugawika katika matawi mawili pekee hivi ni kusema kuwa KN hakiwezi kuzalisha matawi matatu. (Radford 2004)

Utafiti huu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa ambayo inaendana na mada ya utafiti imemsaidia mtafiti kubaini aina za virai vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa na kuvianisha kwa kuzingatia miundo yake na pia kuvichangua kwa kutumia njia ya matawi ambapo kifundo kimoja kiwegawika mara mbili. Hivyo nadharia hii imekuwa ni dira katika uchanganuzi wa kirai cha kibantu mfano kutoka kirai cha Kinyakyusa.

2.5 Hitimisho

Ili kazi hii ya utafiti ikamilike, mtafiti ameangalia maandishi ya wataalamu mbalimbali waliozungumzia kuhusu mada husika. Mtafiti amepitia vitabu mbalimbali, makala na tafiti zilizokwisha fanyika juu ya mada hii ambavyo vimesaidia katika kubaini pengo la utafiti na kumwongezea data katika utafiti huu.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaonyesha mbinu iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu. Imeelezea kwa ufasaha mbinu za ukusanyaji data, vyanzo vya utafiti, vifaa vya utafiti, sampuli na usampulishaji, mkabala uliotumika kukusanya na kuchambua data katika utafiti huu, mawanda ya utafiti, usanifu wa utafiti na changamoto zilizojitokeza wakati wa ukusanyaji data.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika mkoani Mbeya katika wilaya ya Kyela kata ya Ipinda kijiji cha Ipinda. Wilaya ya Kyela ilichaguliwa kwa sababu ni eneo ambalo mtafiti anauzoefu nalo na ni eneo ambalo linawazungumzaji wengi wazawa wa lugha ya Kinyakyusa ambao hawajaathiriwa zaidi na lugha nyingine. Hivyo ilikuwa rahisi kwa mtafiti kupata data halisi.

3.3 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data kama anavyoeleza Adam (2008) ni vielelezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo. Data za msingi (awali) kama anavyozieleza Kothari (2004) ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza uwandani. Data hizi zimekusanywa wakati mtafiti yuko uwandani katika kijiji na sehemu zilizoteuliwa. Data hizo ndizo zimejibu maswali ya utafiti. Data hizo zilinukuliwa kwenye madaftari na vinasauti vimetumika kwa ajili ya kurikodi taarifa.

Data za upili ni zile ambazo tayari zilishakusanywa na zimeshatumika na zimehifadhiwa Kothari (1990). Data hizo pia mtafiti amezipata kupitia maandiko ya wataalamu mbalimbali pamoja na ripoti za aina tofauti. Taarifa hizo pia zimekusanywa kwa kuangalia kazi zilizopita kuhusiana na mada kwa kuangalia vitabu, majarida, na mashapisho na tafiti mbalimbali katika maktaba ya East Africa na Makavazi zilizoko katika Chuo Kikuu ya Dar es Salaam na kwenye mitandao. Kothari (1990) anaifafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Aidha mtaalamu huyu anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data.

Utafiti huu ulitumia mbinu mbili katika ukusanyaji data. Mbinu hizi zimetumika ili kukamilishana na kutoa matokeo ya utafiti yanayohitajika kwa sababu kila mbinu ina mapungufu yake na haiwezi kutoa matokeo yanayojibu maswali ya utafiti. Hivyo, ili kupata matokeo yanayojibu maswali ya utafiti, mtafiti ametumia mbinu ya usaili/mahojiano na mbinu ya ushiriki.

3.3.1 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa wasailiwa. Usaili uliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili na Kinyakyusa. Maswali yaliulizwa yanayohusiana na tungo kirai cha Kinyakyusa, yalijibiwa kwa njia ya mdomo kwa wakati huo huo na hatimaye mtafiti alirekodi majibu hayo katika tepu ya kurekodi na kuandika katika daftari la kumbukumbu. Kwa mujibu wa Kothari (kishajatwa) mbinu hii inaruhusu

unyumbukaji katika mchakato wa kuuliza maswali. Na hatimaye husaidia kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watu wanaoulizwa maswali. Pia inasaidia kupata taarifa za ziada na za kina zaidi hususani pale ambapo majibu ya watu wanaosailiwa yanapokuwa hayaeleweki. Vile vile Kothari anaendelea kueleza kuwa mbinu hii inamruhusu mtafiti kuuliza maswali ya ziada. Vile vile usaili unatusaidia kugundua mahusiano magumu katika mahusiano ya kijamii na hivyo kutuwezesha kuwa karibu na watoa habari. Hivyo basi, katika utafiti huu mbinu ya usaili ilitumika zaidi ili kupata data zinazohusiana na virai cha Kinyakyusa. Mbinu hii ilitoa fursa ya kufafanua maswali pale ambapo mtafitiwa hakuelewa. Pia ilitoa fursa ya watafitiwa waliosoma na wasiosoma kushiriki katika kutoa taarifa.

3.3.2 Mbinu ya Ushiriki

Ni mbinu ambayo mtafiti alikusanya taarifa kwa kushiriki katika mazingira halisi. Adam (2008) anasema kuwa matumizi ya mbinu hii ni lazima mtafitiwa awepo kwenye eneo la utafiti ili kupata taarifa kwa usahihi, ni lazima atumie viungo vya hisia iliwemo kuona kusikia, kugusa, kunusa na kuonja. Ili ushiriki uwe wenye kuleta mafanikio, mtafiti atakuwa makini katika kuandika taarifa, kuvifikia vipengele vyote anavyotaka kushiriki na kuwa na muda wa kutosha. Manufaa ya mbinu hii ni kuwa mtafiti anapata ufahamu wa kina kuhusiana na mada anayoitafiti, pia huielewa vyema jamii anayoifanyia utafiti. Utafiti huu alitumia mbinu hii ya ushiriki katika ukusanyaji wa data. Mtafiti alishiriki katika mazingira halisi ili kupata taarifa kwa usahihi. Alitumia viungo vya hisia kama vile kusikiliza kwa makini majibu ya watafitiwa walipotamka virai vya Kinyakyusa, na kwa njia hii maswali yaliulizwa na majibu ya watafitiwa yalirekodiwa na kuandikwa.

3.4 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti hatavitumia katika ukusanyaji wa data (Kothari 2004). Utafiti huu umetumia vifaa kama vile kinasa sauti kurekodi maelezo, majibizano na mahojiano mbalimbali kati ya mtafiti na watafitiwa ambayo yamemsaidia mtafiti katika uandikaji wa tungo kirai cha Kinyakyusa. Kamera kwa lengo la kupiga picha baadhi ya matukio ili kumsaidia msomaji wa utafiti huu kuelewa vema kile kilichokusudiwa katika utafiti huu kwa ajili ya kumbukumbu na zitakuwa msaada kwa watafiti wengine pale watakapotaka kufanya utafiti katika maeneo hayo. Shajara pia ilitumika katika kuandika data mbalimbali zilizopatikana katika utafiti pamoja na kompyuta katika utayarishaji wa data za utafiti na kinyonya data.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

3.5.1 Sampuli

Kothari (2009) Sampuli ni sehemu ndogo ya populesheni kuu ambayo huteuliwa na mtafiti ili itumike katika utafiti wake. Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwahoji watu wote wanaozungumza lugha ya Kinyakyusa mtafiti alilazimika kufanya uteuzi wa sampuli ili kupata kundi dogo la watu katika wilaya ya Kyela, kata ya Ipinda watafafanyiwa utafiti ambalo limewakilisha kundi kubwa katika kujibu maswali ya utafiti. Kothari anaendelea kufafanua kuwa, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika populesheni kuu ambalo kwalo mtafiti hupata data za utafiti zinazojibu maswali yake ya utafiti. Katika utafiti huu, sampuli ilikuwa ni watu kumi (10) ambao miongoni mwao walikuwa ni Walimu, Wanafunzi na

Wazawa wa lugha ya Kinyakyusa. Sampuli hii pia iliteuliwa kwa kuzingatia uelewa wa watafitiwa kuhusu dhana ya virai na umilisi wao wa lugha hiyo.

3.5.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa uteuzi wa wahusika wachache kutoka katika populesheni kubwa ambao hutumika katika utafiti. Huu ni mchakato wa kuteua idadi fulani ya watu au vitu kutoka kwenye jamii panapofanyika utafiti kwa maana kwamba vitu au watu walioteuliwa watakuwa na sifa zitakazowakilisha jamii nzima inayofanyiwa utafiti (Orodho na Kombo, 2002). Naye Kothari (2004) anasema kuwa usampulishaji ni mpango wa kuchagua sampuli maalumu kutoka katika kundi kubwa. Trochim (2006) anasema kwamba usampulishaji ni mchakato wa kuteua watafiti kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa kwa ajili ya kutoa taarifa ambazo mtafiti huzitumia katika kutoa mahitimisho ya jumla yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa wake. Katika utafiti huu mtafiti alitumia usampulishaji nasibu tabakishi. Usampulishaji nasibu tabakishi ni mbinu ambayo humsaidia mtafiti kupata watafitiwa wale anaowataka kwa uwakilishi sawa kwa kila kundi. Uteuzi huu wa mbinu ufanya sampuli zote katika eneo la utafiti kuwa na haki sawa ya kuchaguliwa kufanya sampuli ya utafiti (Bryman 2004). Katika utafiti huu mtafiti alichagua kutumia usampulishaji nasibu tabakishi ili umsaidie kupata sampuli katika uwakilishi sawa wa makundi mbalimbali. Katika aina hii ya usampulishaji, jumla ya watafitiwa 10 waligawanywa sawasawa kwa kuzingatia kigezo cha elimu (watafitiwa watano wenye kiwango cha elimu ya sekondari na kuendelea na watafitiwa watano wasio na elimu). Idadi hii ya watafitiwa iliteuliwa kwa sababu ni idadi inayotosheleza kutoa matokeo yanayoaminika kutokana na uteuzi sahihi wa

watafitiwa. Pia mtafiti alichagua sampuli hii kutokana na muda mfupi alionao wa kukamilisha utafiti huu kwa wakati. Watafitiwa hao 10 waligawanywa sawa kwa kwa kigezo cha elimu kwa kuzingatia usawa wa idadi ili kubaini aina za virai vya Kinyakyusa na kuweza kuvianisha kwa kuzingatia miundo yake.

Jedwali 3.1: Idadi ya Watafitiwa kwa Kuzingatia Umri na Kiwango cha Elimu

Watafitiwa	Idadi	Umri	Kiwango cha Elimu	
			Wasio na Elimu	sekondari
Wazee	6	55 – 75	3	3
Vijana	4	18 – 54	2	2

Chanzo Data za Uwandani (2016)

Aidha, katika kupata sampuli hiyo ya watafitiwa, suala la umri lilizingatiwa ambapo kulikuwa na makundi mawili, wazee sita (6) na vijana wanne (4). Sababu ya kuchagua makundi mchanganyiko kwa kigezo cha umri ni kwamba katika kabila hili kuna makundi ya wazee na vijana ambao ni wazawa wa lugha hiyo na idadi kubwa ya wazee ilizingatiwa kwa kuwa ndio hasa watumiaji na waenzi wa lugha za Kibantu kuliko vijana.

Pia kigezo cha elimu na umilisi wa lugha ya Kinyakyusa kilizingatiwa katika uteuzi huo wa sampuli kwa sababu taaluma ya sintaksia ya uchanganuzi wa Virai inahitaji uwelewa hivyo basi, walimu watatu (3) na wanafunzi wawili (2) wa Sekondari wenye uwelewa kuhusu virai waliteuliwa katika sampuli hiyo.

3.6 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu umebainisha, kuanisha na kuchanganua virai nomino (KN) na virai (KT) vya Kinyakyusa. Uchunguzi huu umebainisha aina za virai, miundo ya virai hivyo na

kuvichanganua. Ili kufikia malengo ya utafiti huu, mtafiti alitumia mkabala wa kimaelezo. Huu ni mkabala unaotumia maelezo kuelezea jinsi watu wanavyofikiria na kuhisi kuhusu kitu au jambo fulani (Kothari 1990). Mkabala huu wa kimaelezo ni mzuri kuutumia pale unapokusanya taarifa kuhusu mawazo ya watu, mitazamo yao, tabia zao na masuala ya kijamii. Mkabala wa kimaelezo ulitumika zaidi katika ubainishaji wa aina za virai vya Kinyakyusa, uainisha wa virai hivyo kwa kuzingatia miundo yake na uchanganuzi wa virai viwili yaani virai nomino (KN) na virai kitenzi (KT) kwa kutumia nadharia ya X-baa.

3.7 Maadili ya Utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu, ni lazima mtafitiwa aelezwe maadili ya utafiti ili aweze kutoa taarifa za ukweli na uhakika. Aeker (2002) kama alivyonukuliwa na Adam (2008), wametaja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hakutoa siri za watafitiwa. Pia ameeleza haki ya watafitiwa kuhakikishiwa usalama wao, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali waliopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Mtafiti alitambua haki zote hizi na kuzitekeleza. Watafitiwa walijibu maswali waliyopenda kujibu. Tatizo lolote litakalotokea litakuwa ni juu ya mtafiti mwenyewe.

3.8 Changamoto Zilikazojitokeza Wakati wa Ukusanyaji Data

Katika mchakato wa ukusanyaji data kwa kutumia mbinu ya mahojiano, mtafiti alikutana na changamoto mbalimbali. Changamoto zilizojitokeza ni baadhi ya watafitiwa kukataa kutoa baadhi ya taarifa kwa kudhani kuwa mtafiti atafaidika na

kazi hiyo. Hivyo basi, ili kutatua tatizo hilo, mtafiti aliwaonesha watafitiwa kitambulisho chake cha uanafunzi, kibali cha kufanya utafiti na pia aliwaelimisha watafitiwa wake kuwa utafiti wake ni wa kitaaluma na hauhusiani na masuala ya kibiashara.

Changamoto nyingine aliyokabiliana nayo mtafiti kwa njia hii ya mahojiano ni katika swali linalohusu watafitiwa kueleza baadhi ya maana za tungo za lugha zao kwa Kiswahili. Swali hili lilileta ugumu huo, mtafiti alijitahidi kutumia mkalimani ilipobidi kufanya hivyo.

Pamoja na changamoto zote zilizojitokeza katika mchakato wa ukusanyaji data, bado haukuathiri upatikanaji wa data za kutosha kutoka kwa watafitiwa. Hivyo basi, mtafiti aliridhika na data iliyokusanywa kwani ilikidhi malengo ya utafiti.

3.9 Hitimisho

Sura hii kwa ujumla imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika kupata data, eneo la utafiti, sampuli lengwa na mbinu iliyotumika kuwasilisha data zilizokusanywa toka uwandani. Mtafiti aliridhika na data aliyokusanywa uwandani kwa sababu imekidhi malengo ya utafiti. Kwa hiyo data zote zilizokusanywa zimewasilishwa kwa upana katika Sura ya Nne.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data zilizopatikana katika eneo la utafiti. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya X-baa ambapo virai huchanganuliwa kwa kuzingatia kategoria na kila kirai humilikiwa na kichwa leksika. (Haegeman,1991).

Uchambuzi huu wa data umelenga kujibu maswali ya utafiti huu na kuweza kukamilisha malengo ya utafiti. Maswali hayo Kwanza, Je, kirai cha Kinyakyusa hakiweze kubainishwa?, Pili, Je, kirai cha Kinyakyusa hakiwezi kuainishwa kwa kuzingatia miundo yake? Tatu, Je, kirai hiki cha Kinyakyusa hakiwezi kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa?

Sura hii imechambuliwa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza kubainisha virai vya Kinyakyusa, sehemu ya pili kuanisha virai hivyo kwa kuzingatia miundo yake, sehemu ya tatu kuchanganua virai viwili yaani kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) vya Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa, na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Uchambuzi wa data umehusishwa na malengo mahsusi ya utafiti na kwa kujibu maswali ya utafiti baada ya kuzikusanya na kuzichanganua data zilizopatikana kwa kutumia nadharia ya X-baa.

4.2 Kubainisha Virai vya Kinyakyusa

Haegeman (1994) anadai kuwa kulingana na nadharia hii ya X-baa virai vyote

vinatawaliwa na neno kuu yaani X. Maneno haya makuu ni vitengo vya chini kabisa na hutawala maneno mengine. Radford (1988) naye anasema, kila kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai chote, na huainishwa kimuundo kulingana na neno kuu/kichwa cha kirai husika. Kirai ambacho neno lake kuu ni nomino/ au kiwakilishi huitwa kirai nomino, kwa mfano: *Mtoto huyu*. Hapa neno kuu ni mtoto, ndipo kirai hicho kikaitwa kirai nomino. Maelezo hayo yamemsaidia mtafiti katika kubaini virai vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa kwa kuzingatia sifa ya kirai husika. Navyo vinabainishwa kama ifuatavyo:

Kinyakyusa

Kiswahili

i) Kirai Nomino (KN)

inyumba kanunu
Roza akafika
Ilisyu Iya Bumi
Ummanyiisi gwa Kiswahili
Uhiji

nyumba nzuri
Roza hajafika
neni la Mungu
mwalimu wa Kiswahili
mwizi

ii) Kirai Kivumishi (KV)

Umkota jula mkamu -
Ukisu kinywamu
Undumiana unskari
Uhiji nkulumba pakijiji
Igorofa itali lyelu

mzee yule mjanja
nchi kubwa
kijana mwanajeshi
mwizi mkubwa kijijini
gorofa refu jeupe

iii) Kirai Kitenzi (KT)

Bhosa bhasokilepo nulubhunju
Balilemo bo kakali akababilo
Untumigwa asikukusokapo lilino
Ali gwa sukulu
Une nakatele ukwenda

Wote waliondoka asubuhi sana
Walikula kabla ya muda
mjumbe haondoki leo
alikuwa mwanafunzi
mimi nilichoka kutembea

iv) Kirai Kielezi (KE)

Mbimbibi asokile
Lilino nulubhunju afikile
Igari ibofu kabisa
Inyanja inunu fiyo
Ikitwalo kisito fiyo

aliondoka haraka haraka
leo asubuhi amefika
gari bovu kabisa
ziwa zuri sana
mzigo mzito mno

v) **Kirai Kihusishi (KH)**

<i>Bhabukile kwa mjomba nulubhunju</i>	<i>walikwenda kwa mjomba asubuhi sana</i>
<i>Mbepo gwa Kyala</i>	<i>Roho wa Mungu</i>
<i>Pitasi bo asokilepo umwene</i>	<i>baada ya yeye kuondoka</i>
<i>Asikusokapo mpaka kilabo</i>	<i>haondoki hadi kesho</i>
<i>Ikitabu ikinywamu kya Kiswahili</i>	<i>kitabu kikubwa cha Kiswahili</i>
<i>Umwenda inyali fijo</i>	<i>nguo chafu sana</i>

Mifano iliyotolewa hapo juu ni mifano ya virai mbalimbali vya Kinyakyusa ambavyo vimekitwa katika neno kuu yaani N, V, T, E na H. Hii ina maana kwamba katika virai namba (I –V), maneno yaliyoandikwa kwa hati ya kulala ndio chimbuko la uhusiano uliopo katika maneno yote yanayohusika katika kila kirai. Hivyo basi ubainishaji huu wa kirai cha Kinyakyusa unadhihirisha kuwa tungo kirai cha Kinyakyusa kina maumbo na miundo mbalimbali kulingana na virai vilivyomo katika lugha hiyo.

4.3 Kuainisha Virai vya Kinyakyusa kwa Kuzingatia Miundo Yake

Katika utafiti huu uainishaji wa virai vya Kinyakyusa umezingatia kigezo cha kimuundo ambapo tungo kirai hiki huhusisha neno moja au zaidi ambayo huwekwa pamoja katika mpangilio maalumu unaozingatia uhusiano uliopo baina ya neno kuu na maneno mengine. Radford (kishatajwa) anadai kuwa, uainishaji wa virai kimuundo hutegemea neno kuu katika kirai hicho. Maelezo ya mtalaamu huyo yalimsaidia mtafiti wa utafiti huu katika uainishaji wa virai vya Kinyakyusa kwa kuzingatia miundo yake na kuweza kubaini miundo tofauti ya virai hivyo kama ifuatavyo:

4.3.1 Kirai Nomino (KN)

Massamba na Wenzake (kishatajwa) Kirai nomino ni kirai ambacho muundo wake

umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno mengine. Muundo wa kirai nomino cha Kinyakyusa umejikita katika mahusiano maalum baina ya neno kuu na maneno mengine. Kirai nomino hiki hutawaliwa na nomino au viwakilishi vyake ambavyo ndivyo vichwa vyake. Miundo hiyo ya Virai inajitokeza kama ifuatavyo:

Nomino pekee (N)

Ni kirai kinachoundwa na nomino pekee. Kamusi ya Longhorn (imeshatajwa) inasema kirai ni kipashio cha kisafuri kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano na kimuundo na kiima na kiarifu. Kwa mfano:

Kyala - Mungu

Ikisu - dunia

Omwana - mtoto

Ikigoda - kiti

Amesi - maji

Nomino na kivumishi (N+V)

Ni muundo mwingine wa kirai nomino cha Kinyakyusa ambacho uundwa na nomino kama kichwa cha kirai na kuambatana na kivumishi katika kukijenga. Kwa mfano:

Umpiki untali - Mti mrefu

Umpiki = nomino

Untali = kivumishi

Kyala gwetu - Mungu wetu

Kyala = nomino

Gwetu = kivumishi

Igari gwake – gari lake

Igari = nomino

Gwake = kivumishi

Tata gwenu = baba yenu

Tata = nomino

Gwenu = kivumishi

Imienda minyali - nguo chafu

Imienda = nomino

Minyali = kivumishi

Nomino na Kivumishi (kiwakilishi) (N+V)

Kirai hiki hutawaliwa na neno kuu “nomino” au “kiwakilishi chake” na kuambatana na kivumishi katika kukikamilisha. Kwa mfano:

Jula unkulumba - yeye mkubwa

Jula = kiwakilishi

Unkulumba = kivumishi

Gwangu mnunu - wakwangu mzuri

gwangu = kiwakilishi

mnunu = kivumishi

Jila inandi - ile ndogo

Jila = kiwakilishi

inandi = kivumishi

Jula mololo = Yeye mpole

Jula = kiwakilishi

Mololo = kivumishi

Jula gwangu - yeye wangu

Jula = kiwakilishi

Gwangu = kivumishi.

Nomino ya kitenzi jina na kivumishi (N+V)

Katika uuundo huu wa kirai nomino, kitenzi jina ndicho chimbuko la mahusiano na maneno mengine katika kukiuunda. Mfano katika virai vifuatavyo:

Ukwimba panywamu - Kuimba kuzuri.

Ukwimba = nomino ya kitenzi (kitenzi nomino)

Panywamu = kivumishi

Ukwenda gwake - kutembea kwake

Ukwenda = kitenzi nomino

Gwake = kivumishi

Kujoba panandi - kuongea taratibu

Kujoba = kitenzi nomino

Panandi = kivumishi

Ukumanyisye ikiswahili mbombo ingavu - *kufundisha Kiswahili ni kazi ngumu*

Ukumanyisye = kitenzi nomino

Ikiswahili = kivumishi nomino kinachovumisha nomino nyingine iliyoitangulia
(Masebo 2007:127-129 na Mkajile 2008: 20)

Usyiganile kununu - *kupenda kuzuri*

Usyiganile = kitenzi nomino

Kununu = kivumishi.

Nomino na nomino (N+N)

Katika muundo huu wa kirai nomino, nomino mbili ndizo chimbuko la mahusiano

baina kichwa na mafungu mengine ya maneno. Mfano katika virai vifuatavyo:

Ikyindi gwa imbene - *Ugali kwa mbuzi.*

Ikyindi = nomino

Gwa = kihusishi

Imbene = nomino

Nsyiganile ihalale pamo ikyindi - *napenda ndizi au ugali*

Ihalale = nomino

Pamo = kiunganishi

Ikyindi = nomino

Ikyai ni kisyesye - *chai na mkate*

Ikyai = nomino

Ni = kiunganishi

Kisyesye = nomino

Abakangale ni abakeke - *wazee na vijana*

Abakangale = nomino

Ni = kiunganishi

Abakeke = nomino

Tata ni juba - *baba na mama*

Tata = nomino

Ni = kiunganishi

Juba = mama

Nomino na kivumishi na kivumishi (N+V+V)

Huu nao ni muundo unaojitokeza katika kirai nomino cha Kinyaktyusa ambapo neno

kuu ni nomino kikiambatana na vvimishi viwili katika kukijenga. Mfano:

Ugwasukulu mnini mmaganyi - Mwanafunzi mdogo mtundu.

Ugwasukulu = nomino

Mnini = kivumishi₁

Mmaganyi = kivumishi₂

Ummanyisi John nkali - mwalimu John mkali

Ummanyisi = nomino

John = kivumishi jina kinachoivumisha nomino iliyoitangulia₁ (Masebo 2008:127)

Nkali = kivumishi₂

Igorofa lyelu itali - gorofa jiupe refu

Igorofa = nomino

Lyelu = kivumishi₁

Itali = kivumishi₂

Unkikulu unditu gwa kisu kya Tanzania - mwanamke mweusi Mtanzania

Unkikulu = nomino

Unditu = kivumishi₁

Gwa kisu kya Tanzania = kivumishi₂

Unyambala untali nsekale - mwanaume mrefu mwembamba

Unyambala = nomino

Untali = kivumishi₁

Nsekale = kivumishi₂

Nomino na kivumishi na Kielezi (N+V+E)

Ni muundo mwingine wa kirai hiki cha Kinyaktyusa kinachouundwa na neno kuu

nomino na kuambatana na vifungu vingine vya maneno . kwa mfano katika virai

vifuatavyo:

Igali inywamu fijo - Gari kubwa sana.

Igali = nomino

Inywamu = kivumishi

Fijo = kielezi

Omwana nnini fijo - mtoto mdogo sana

Omwana = nomino
 Nnini = kivumishi
 Fijo = kielezi

Ijiko ibofu kangi - jiko bovu tena
 Ijiko = nomino
 ibofu = kivumishi
 kangi = kielezi

Irangi nditu fijo - rangi nyeusi mno
 Rangi = nomino
 Nditu = kivumishi
 Fijo = kielezi

Ibegi sito ukukinda - begi zito zaidi
 Ibegi = nomino
 Sito = kivumishi
 Ukukinda = kielezi

Nomino Pamoja na Kirai Husishi (N + KH)

Muundo huu wa kirai nomino pia hujitokeza kaktika kirai hiki cha Kinyakyusa ambapo neno kuu ni nomino anayoambatana na kihusishi katika kukijenga. Kwa mfano:

Omwana gwa tata - Mtoto wa baba.
 Omwana = nomino
 Gwa = kihusishi
 Tata = nomino

Ilisyu kya Bumi - Neno la Mungu
 Ilisyu = nomino
 Kya = kihusishi
 Bumi = nomino

Mbepo gwa Kyala = Roho wa Mungu
 Mbepo = nomino
 Gwa = kihusishi
 Kyali = nomino

Roza mpaka lilino akalipo = Roza mpaka leo yupo
 Roza = nomino
 Mpaka = kihusishi
 Lilino akalipo = kirai kielezi

Nomino na Kishazi Tegemezi (N+KTg)

Muundo huu wa kirai nomino hujengwa na neno kuu nomino na kikiambatana na kishazi tegemezi katika kukikamisha. Kwa mfano katika virai nomino vifuatavyo vya

Kinyakyusa:

Umwana ujugwalimbwene jo mwanangu - Mtoto uliyemwona ndiye mwanangu.

Umwana = nomino

Ujugwalimbwene = kishazi tegemezi

Igari ili ligwile mmajolo lisosigwepo - *gari lililoanguka jana* limeondolewa

Igari = gari

Ili ligwile mmajolo = kishazi tegemezi

Umundu ujuikutila asokepo - mtu aliyemwoga aondoke

Umundu = (Mtu)- nomino

Ujuikutila = (aliyemuona)- kishazi tegemezi

Ukwisi ulutwatekile mmajoro - mto uliojaa jana

Ukwisi = mto

Ulutwatekile = kishazi tegemezi

Kibainishi, Nomino na Kivumishi (KIB+ N+V)

Kibainishi ni maneno yanayo bainisha au kutilia mkazo nomino inayofuata au inayofuatwa. Rubanza (2003) kwa mfano katika kirai nomino hiki cha Kinyakyusa.

ugu un kikulu untengamojo fijo - *huyu mwanamke mnyenyekevu sana.*

ugu = kibainishi

Unkikulu = nomino

Untengamojo fijo = kivumishi

Ikarata iki kinandi - *kitabu hiki kidogo*

Iki = kibainishi

Ikarata = nomino

Kinandi = kivumishi

Jula Juma Nsomari = *Yule Juma nsomari*

Jula = kibainishi

Juma = nomino

Nsomari = kivumishi

Uju Kyala gwitu - huyu Mungu wetu

Uju = kibainishi

Kyala = nomino

Gwitu = kivumishi

4.3.2 Kirai Kitenzi (KT)

Kitenzi kulingana na Kihore na Wenzake (2001) ni aina ya neno ambalo linatoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalitendwa na kiumbe au kitu. Kirai tenzi ni neno ama fungu la maneno ambalo huwa na kitenzi kama kichwa cha kirai.

Rubanza (2003) anasema kwamba, kitenzi ndio msingi mkuu wa sentensi. Kitenzi kimoja kinaweza kuwa ni sentensi kamili. Pia anataja aina za vitenzi; vitenzi elekezi na vitenzi sielekezi ambavyo havihitaji yambwa. Anaendelea kwa kusema kuwa, Kirai kitenzi kinaweza kuambishwa viambishi awali na viambishi tamati vya kauli na dhamira. Katika utafiti huu mtafiti amejikiita zaidi katika kuchunguza miundo ya virai tenzi vya Kinyakyusa. Kirai kitenzi cha Kinyakyusa kinaweza kuwa pekee au ufuatwa na kijalizo cha virai elezi ama virai vihusishi au nomino hasa katika vitenzi vishirikishi. Maelezo haya yalisaidia katika utafiti huu kubaini vitenzi vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa kama ifuatavyo:

- i) Virai vitenzi vikuu
- ii) Virai vitenzi visaidizi na
- iii) Virai vitenzi vishirikishi.

4.3.2.1 Virai Vitenzi Vikuu (T)

Vitenzi vikuu katika sentensi za Kinyakyusa ndivyo chimbuko la mahusiano baina ya kichwa na maneno mengine. Vitenzi hivi vingi vimeambishwa mofu za viambishi

awali na hubeba maana kuu ya kitenzi. Miundo ya vitenzi vikuu hivi hujitokeza kama ifuatavyo:

Kitenzi Kikuu Pekee (T)

Katele - choka

Joba - sema

kwimba - imba

bhakuiputa kukipanga - *wanaomba* kanisani

atupele imyenda - *ametupa* nguo

Mifano ya hapo juu, inatuonyesha vitenzi vikuu pekee vilivyoambishwa mofu za viambishi awali na vitenzi vinajitokeza vikiwa pekee pasipo kutanguliwa na viambishi awali alhali vikifuatiwa na maneno mengine.

Kitenzi na Nomino (T+N)

Twalimmwambilike umwana - *tulimpokea mtoto*

twalimmwambilike = kitenzi halisi / kitenzi elekezi.

umwana = nomino.

Abhonile ikisu - *ameona dunia*

Abhonile = kitenzi elekezi

ikisu = nomino

Jikutilisya ingisi - *linatisha giza*

Jikutilisya = kitenzi

Ingisi = nomino

Igari libigwe kukyela - *gari limeibiwa Kyela*

Libigwe = kitenzi

kuKyela = nomino

ukwimba Loveness - *anaimba Loveness*

ukwimba = kitenzi

Loveness = nomino

Kitenzi na Nomino na Kirai Vumishi (T+N+V)

John atwale igari inywamu - *John alileta gari kubwa*

Atwale = kitenzi elekezi

igari inywamu = kirai nomino

igari = nomino

inywamu = kivumishi.

Amenye kukaja mnyako - anafhamu nyumbani kwako

Amenye = kitenzi
 Kukaja = nomino
 mnyako = kirai vuminishi

fyatwaligwe ifyombo bhosa - ilichukuliwa mizigo yote

fyatwaligwe = kitenzi
 fyombo = nomino
 bhosa = kivumishi.

Pakilabo isege ummanyisi gwako - Kesho aje mwalimu wako

isege = kitenzi
 ummanyisi = nomino
 gwako = kivumishi

Ikumanyisye ikiswahili kanunu - anafundisha Kiswahili vizuri

Ikumanyisye = kitenzi
 Ikiswahili = nomino
 Kanunu = kirai vumishi.

Kitenzi na Nomino na Kirai Kielezi. (T+N+KE)

Ikulonda imbombo inunu - anatafuta kazi nzuri

ikulonda = kitenzi elekezi
 imbombo = nomino
 Kirai kielezi = inunu

Nilile isyati lyelu - nimenunua shati jeupe

Nilile = kitenzi
 Isyati = nomino
 Lyelu = kielezi

Lyasokile ilisyu kanunu - ilisikika sauti nzuri

Kitenzi = lyasokile
 Nomino = ilisyu
 Kielezi = kanunu

Inguku jitelile amafumbi pasi pa umpiki - kuku ametanga mayai chini ya mti

Kitenzi = jitelile
 Nomino = amafumbi
 Kirai kielezi = pasi pa umpiki

Umbulege ungwe mnywamu - umweleze wewe taratibu

Kitenzi = umbulege
 Kiwakilishi = wewe
 Kirai kielezi = mnywamu.

Kitenzi na Kirai Nomino na Kirai Husishi (T+N+KH)

Tata gwao *Atwele imbene gwa mjomba* - baba yao *alileta mbuzi kwa mjomba*

Atwale = kitenzi elekezi.

Imbene gwa mjomba = kirai nomino.

gwa mjomba = kirai husishi.

gwa = kihusishi

mjomba = nomino.

Pakilo *fyatwaligwe ifyombo ni basi* - usiku *ulisafirishwa mzigo kwa basi*

Fyatwaligwe = kitenzi elekezi

Ifyombo ni basi = kirai nomino

ni basi = kirai kihusishi

ni = kihusishi

Basi = nomino

Ajobile inongwa ja Kyala - *aliongea neno la Mungu*

Ajobile = kitenzi kikuu

Inongwa ja Kyala = kirai nomino

Ja Kyala = kirai kihusishi

Ja = kihusishi cha a-unganifu

Kyala = nomino

Pakilabo kilo Rose *apigile imbatata ifya Uyole* - jana usiku Rose *alipika viazi mvirigo vya Uyole*

Apigile = kitenzi kikuu

Imbatata ifya Uyole = kirai nomino

Ifya Uyole = kirai kihusishi

Ifya = kihusishi

Uyole = nomino

Yohana ni Damas *wapele imbombo ku nogwa gwangu* - *wamepatiwa kazi kwa ajili yangu*

Wapele = kitenzi kikuu

Imbombo ku nogwa gwangu = kirai nomino

Ku nongwa gwangu = kirai kihusishi

Ku nongwa = kihusishi cha sababu

Gwangu = kiwakilishi

Kitenzi na Kirai Kielezi (T+KE)

Afikile nulubhunju - *alifika mapema*

Afikile = kitenzi

Nulubhunju = kirai kielezi

Bhana *babujile kang* - *watoto walirudi tena*

Kitenzi = babujile

Kirai kielezi = kang

Bhosa *tukwaganile kabili kabili* - wote *tunakutana mara kwa mara*
 Kitenzi = tukwaganile
 Kirai kielezi = kabili kabili

Bhahesya *balilemo isaa sita pamusi* - wageni *walikula saa sita mchana*
 Balilemo = kitenzi
 Isaa sita pamusi = kirai kielezi

Mariana *akafika lilino* - Mariana *hajafika leo*
 Akafika = kitenzi
 Lilino = kirai kielezi.

Kitenzi na kirai vielezi viwili (T+E+E)

Mhesya *asokilepo lilino nulubhunju* - mgeni *ameondoka leo asubuhi*
 asokilepo = kitenzi
 Lilino = kielezi₁
 Nulubhunju = kielezi₂

Samuel *afumile imbombo inunu kangi* - Samuel *amepata kazi nzuri tena*
 Afumile = kitenzi
 Inunu = Kielezi₁
 Kangi = kielezi₂
 Imbeba *jilingile ukutinda nkati* - panya *aliingia zaidi ndani*
 Jilingile = kitenzi
 ukutinda = kielezi₁
 nkati = kielezi₂

Dreva *atwale igari kukaja pakilo* - dreva *alileta gari nyumbani usiku*
 Atwale = kitenzi
 Igari = kirai nomino
 kukaja = kielezi₁
 pakilo = kielezi₂

wahesya *bhasokile nulubhunu fijo* - wageni *waliondoka mapema sana*
 bhasokile = Kitenzi
 nulubhunju = Kielezi₁
 fijo = Kielezi₂

Kitenzi na Kirai Husishi (T+KH+N)

Inyumba jijengwile kifuki ni nyanja = anaishi karibu na ziwa
 jijengwile = kitenzi elekezi
 kifuki na = kirai husishi
 Kifuki na = kihusishi
 Nyanja = nomino

Ivindu *Fyatwaligwe ni igari inywamu* - vitu *ilisafirishwa kwa gari kubwa*

Fyatwaligwe = Kitenzi

Ni igari inywamu = Kirai kihusishi

Ni = Kihusishi

Igari inywamu = Nomino na kivumishi yake.

Omwana *Atugesye kifuki nu moto* - *mtoto ameketi karibu na moto*

Atugesye = Kitenzi

Kifuki nu moto = Kirai kihusishi

Kifuki nu = Kihusishi

Moto = Nomino

Mmanyani gwangu *alyilile mpaka pakilo* - rafiki yangu *alilia hadi usiku*

Alyilile = Kitenzi

Mpaka pakilo = Kirai kihusishi

Mpaka = Kihusishi

Nomino = pakilo

Unkonta *atugesye pasi pa umpiki* - mzee *ameketi chini ya mti*

Atugesye = kitenzi

Pasi pa mpiki = kirai kihusishi

Pasi pa = kihusishi

Umpiki = nomino

Kitenzi na Kihusishi na Kivumishi (T+KH+KV)

Unkukilu jula *ajobile jo mnyake* - mwanamke yule *aliongea ya kwake*

Ajobile = Kitenzi

Jo mnyake = Kirai kihusishi

Jo = Kihusishi cha a-unganifu

Mnyake = Kivumishi

Mama *apijile fya mmyetu* - mama *amepika vya kwetu*

Apijile = Kitenzi

fya mmyetu = Kirahi kihusishi

fya = Kihusishi

Mmyetu = kivumishi

Umputi gwitu *aputile kunongwa gwangu* - mchungaji wetu *aliomba kwa ajili yangu*

Aputile = Kitenzi

Kunongwa gwangu = Kirai kihusishi

Kunongwa = Kihusishi

Gwangu = Kivumishi

Inkindu *Inyelile pa mwanya mnywamo* - kitu *kiliruka juu yao*

Inyelile = Kitenzi

Pa mwanya mnywamo = Kirai kihusishi

Pa mwanya = Kihusishi
Mnywamo = Kivumishi

Kitenzi na Krai kihusishi na kirai Kielezi (KT+KH+KE)

Ambonile pabhutali fijo - alimwona kwa mbali sana

Ambonile = Kitenzi
Pabhutali fijo = Kirai kihusishi
Pabhutali = Kihusishi
Fijo = Kielezi

Rose akafika ukufuma nulubhunju - Rose hajaondoka tangu asubuhi

Akafika = kitenzi
Ukufuma nulubhunju kirai kihusishi
Ukufuma = kihusishi
Nulubhunju = kielezi

Mhesya asikusokapo mpaka kilabo - mgeni haondoki mpaka kesho

Asikusokapo = kitenzi
Mpaka kilabo = kirai kihusishi
Mpaka = kihusishi
Kilabo = kielezi

Ilisye lyasokile pabhutali fijo - sauti ilisikika kwa mbali sana

Lyasokile = kitenzi
Pabhutali fijo = kirahi kihusishi
Pabhutali = kihusishi
Fijo = kielezi

Bhafikile bo pakali isaa sita pamusi - walifika kabla ya saa sita mchana

Bhafikile = Kitenzi
Bo pakali isaa sita pamusi = Kirai kihusishi
Bo pakali = Kihusishi
Isaa sita pamusi = Kielezi

Kitenzi Kisaidizi na Kitenzi Kikuu (Ts+T)

Kihore na Wenzake (kishatajwa) kitenzi kisaidizi ni kitenzi ambacho kinaambatana na kitenzi kikuu katika sentensi. Kitenzi hiki kinaweza kuwa kitenzi kimoja au viwili zinavyotangulia kitenzi kikuu. Maelezo haya yamesaidia katika utafiti huu kukianisha kirai kitenzi kisaidizi cha Kinyakyusa ambacho huambatana na kitenzi

kikuu katika kukikamilisha. Kitenzi hiki kinaweza kuwa kimoja ama viwili kama ifuatavyo:

Kitenzi Kisaidizi na Kitenzi kikuu Kimoja (Ts+T)

Ugwe *jo* ukwimba - wewe ulikuwa unaimba

Jo = kitenzi kisaidizi

ukwimba = kitenzi kikuu

bhafikile babujile kangi - *walifika wakarudi* tena

bhafikile = kitenzi kisaidizi

babujile = kitenzi kikuu

bhosa bhasokilepo atwelepo igari - *wote waliondoka alipoleta gari*

bhasokilepo = kitenzi kisaidizi

atwelepo = kitenzi kikuu

Ulwisi jo lwaliswile amatope - *mto ulikuwa umejaa matope*

Jo = kitenzi kisaidizi

Lwaliswile = kitenzi kuu

Vitenzi Visaidizi viwili na Kitenzi Kikuu (Ts+Ts+T)

Ingisi *jo* jikutilisya kujatya pakilo - *giza lilikuwa linatisha kutembea usiku*

Jo = kitenzi kisaidizi₁

Jikutilisya = kitenzi kisaidizi₂

Kujatya = kitenzi kikuu

Juma ali kubhuka kuipuita mu kipanga - *Juma alikuwa anakwenda kuomba kanisani*

Ali = kitenzi kisaidizi₁

Kubhuka = kitenzi kisaidizi₂

Kuiputa = kitenzi kikuu

Alyimbile akasokapo kubhuka ulukomano - *aliimba akaondoka kwenda mkutanoni*

Alyimbile = kitenzi kisaidizi₁

Akasokapo = kitenzi kisaidizi₂

Kubhuka = kitenzi kikuu

Wakabangale *gitu bhali bhakafika kutuponya* - *wazee wetu walikuwa hawajafika kutusalimia*

Bhali = kitenzi kisaidizi₁

Bhakafika = kitenzi kisaidizi₂

Kutuponya = kitenzi kikuu

4.3.2.2 Kitenzi kishirikishi (t)

Virai tenzi vishirikishi vya Kinyakyusa ni virai ambavvo huhitaji vijalizo ill viweze kukamilika. Virai hivi huhitaji vijalizo ambavyo vinaweza kuwa nomino, kielezi au kivumishi. Navyo vinajitokeza kama ifuatavyo:

Kitenzi Kishirikishi na Kirai Nomino (t+KN)

Aligwa sukulu - alikuwa mwanafunzi

Kitenzi kisaidizi = ali

Kirai nomino = gwasukulu

Jula ni uhiji - yule ni mwizi

Ni = kitenzi kishirikishi

Uhiji = kirai nomino

John ali ummanyisi - John alikuwa mwalimu

Kitenzi kishirikishi = ali

Kirai nomino = ummanyisi

Mwaipopo ali ntajiri - Mwaipopo alikuwa tajiri

Ali = kitenzi kishirikishi

Ntajiri = kirai nomino

Kitenzi kishirikishi na Kirai Kielezi (t+KE)

Ikibusu jali nkati - choo kilikuwa ndani

Jali = kitenzi kishirikishi

Nkati = kirai kielezi

Pala po pamyabo - pale ndipo kwao

Po = kitenzi kishirikishi

Pamyabo = kirai kielezi

Ichai jiku liliko - chai igali jikoni

Jiku = kitenzi kishirikishi

Liliko = kirai kielezi

Kitenzi Kishirikishi na Kivumishi (t+KV)

Omwana jula ntali jo mwanangu - mtoto yule mrefu ndiye mwanangu

Jo = kitenzi kishirikishi

Mwanangu = kivumishi kimilikishi

Ikikota kyali kinyali - kiti kilikuwa kibofu

Kyali = kitenzi kishirikishi

Kinyali = kirai kivumishi

Sahani jali nyali - sahani ilikuwa chafu

Jali = kitenzi kishirikishi

Nyali = kirai kivumishi

Julieth jo umtengamojo - Julieth ndiye mwema

jo = kitenzi kishirikishi

umtengamojo = kirai kivumishi

4.3.3 Kirai Vumishi (KV)

Masebo (2007) kivumishi ni neno au kikundi cha maneno kinachotoa maelezo zaidi juu ya nomino au kiwakilishi chake. Maelezo hayo yanaweza kuwa ni jinsi nomino inavyotaja ilivyo tabia ya nomino, mahali au idadi ya nomino. Kivumishi hutokea pia kumilikiwa kwa nomino inayotajwa. Maelezo ya mtalaamu huyo yamewezesha mtafiti kubaini kirai kivumishi cha kinyakyusa. Kirai kivumishi hiki cha Kinyakyusa hujikita (hupatikana ndani ya) kirai nomino japo wakati mwingine hupatikana ndani ya kirai tenzi hasa kinapotumika pamoja na kitenzi kishirikishi. Hata hivyo kirai vumishi cha Kinyakyusa huwa na muundo uliobainifu. Kama ifuatavyo:

Kivumishi pekee (V)

Inunu - nzuri

Ingisi sito - giza nene

Sito = kivumishi

Inyumba inywamu - nyumba kubwa

Inywamu = kivumishi cha sifa

Bhasukulu bhosa - wanafunzi wote

Bhosa = kivumishi cha idadi

Injila ndali jikukatasya - safari ndefu inachosha

Ndali = kivumishi cha sifa

Mhesya gwetu - mgeni wetu
Gwetu = kivumishi kimilikishi

Kivumishi na vivumishi vingine (V+V)

imbene gwetu nkamu - mbuzi wetu mjanja
Gwetu nkamu = kirai kivumishi
Gwetu = kivumishi₁
Nkamu = kivumishi₂

Ulwisi ulunandi nntali - mto mdogo mrefu
Ulunandi ntali = kirai kivumishi
Ulunandi = kivumishi₁
Ntali = kivumishi₂

Ingisi sito iji jikutititsya - giza nene ambalo linatisha
Sito iji jikutititsya = kirai kivumishi
Sito = kivumishi
Iji = kivumishi KTg

Kivumishi na Kielezi (V+E)

Bhabukile Iluka inywamu fijo kula kukijiji - Walitembelea duka kubwa sana kule kijijini
inywamu = kivumishi
fijo kula kukijiji = kirai kielezi

Afrika kisu kinywamu fijo - Afrika bara nzuri mno
Kisu kinyamu = kirai kivumishi
Fijo = kirai kielezi

Umundu jula unakali fijo
jula unkali = kirai kivumishi
fijo = kirai kielezi

Ikijiji kinunu kya Kyato - kijiji kizuri cha Chato
Kinunu = kivumishi
Kya Kyato = kirai kielezi

Kivumishi na nomino (V+N)

Abhana bhosa bhabukile gwa mjomba - Watoto wote walikwenda kwa mjomba
gwa = kivumishi cha 'a' unganifu
mjomba = nomino

Umyambala ummanyili fijo - mwanaume msomi sana
msomi = kivumishi

fijo = kirai kielezi

imbene mnywamu fijo jasobhile - mbuzi mkubwa sana amepotea

mnywamu = kivumishi

fijo = kirai kielezi

Kivumishi na Kishazi Tegemezi (V+KTg)

Igali lyelu ili libigwe - gari jeupe ambalo limeibiwa

Lyelu ili = kirai kivumishi

Lyelu = kivumishi

Ili = kishazi tegemezi

Injila isekele jiswile imifwa - njia nyembamba iliyojaa miba

Isekele jiswile = kirai kivumishi

Isekele = kivumishi

Jiswile = kishazi tegemezi

Umyambala unkali ujuamwegile Janeth - mume nkali aliyemwoa Janeth

Unkali ujuamwegile = kirai kivumishi

Unkali = kivumishi

Ujuamwegile = kishazi tegemezi

Ingisi sito iji jikutitisa - giza nene ambalo linatisha

Sito iji = kirai kivumishi

Sito = kivumishi

Iji = kishazi tegemezi

Igari inywamu ili ligwile mmajolo lisosigwepo - gari kubwa lililoanguka jana limeondolewa

Inywamu ili ligwile mmajolo = kirai kivumishi

Inywamu = kivumishi

Ili ligwile mmajolo = kishazi tegemezi.

4.3.4 Kirai Kielezi (KE)

Kirai kielezi cha Kinyakyusa ni neno au kikundi cha maneno yanayofafanua kitenzi,

kivumishi au kielezi kingine. Neno kuu katika kirai hiki ni kielezi. Kinaweza

kinajitokeza katika miundo tofauti tofauti kama ifuatavyo:

- i) Virai elezi vya wakati - pakilo atwele igali = usiku alileta gari
- ii) Virai elezi vya namna - bhajobile kambimbibi – waliongea haraka haraka

- iii) Virai elezi vya mahali – bhabukile pabwifiso bwa finyamana – walitembelea
mbuga ya wanyama
- iv) Virai elezi viulizi - abhukile kugu? – ameenda wapi?
- v) Virai elezi vya kiasi - bhandu ukutima fijo – watu wengi sana

Virai hivi huweza kujitokeza kabla ama baada ya kitenzi. Kwa mfano: “*nulubhunju asokile - asubuhi sana aliondoka*”. Katika sentensi hiyo kielezi kimejitokeza kabla ya kitenzi na “*Mmanyani gwangu abukile kangi - Rafiki yangu aliondoka tena*”. Kielezi kimejitokeza baada ya kitenzi. Virai Vielezi hizi vinaweza kuundwa kwa:

Kielezi pekee (E)

Nulubhunju – asubuhi

Pakilo = usiku

Lilino pamajolo = leo hii jioni

Paitasyi tukumbonana = *baadaye* tutaonana

Vielezi Zaidi ya Kimoja (E+E)

Unkikiulu mnunu fijo - Mwanamke mzuri sana

Mnunu fijo = kirai kielezi

Mnunu = kielezi₁

Fijo = kielezi₂

Ibegi sito ukukinda = begi zito zaidi

Sito ukukinda = kirai kielezi

Sito = kielezi₁

Ukukinda = kielezi₂

Ulwisi lwatekile nulubhunju mmajolo - mto ulijaa jana asubuhi

Nulubhunju mmajolo = kirai kielezi

Nulubhunju = kielezi₁

Mmajolo = kielezi₂

Pala pamyabo kukijiji jonanhike - pale kwao kijijini pameharibika

Pamyabo kukijiji = kirai kielezi

Pamyabo = kielezi₁

Kukijiji = kielezi₂

Kielezi na Kirai Husishi E+KH)

Imbene ilambalile *ichumba pambali pa liliko* - mbuzi alilala chumbani kando ya jiko.

Ichumba pambali pa = kirai kielezi

Ichumba = kielezi

Pambali pa = kirai kihusishi

Bo jikindile isaa sita pamusi ulukomano lwabombigwe - baada ya saa sita mchana mkutano ulifanyika

Bo jikindile isaa sita pamusi = kirai kielezi

Bo jikindile = kirai kihusishi

Isaa sita pamusi = kielezi

Balilemo bo kakali pakilo - walikula kabla ya usiku

Bo kakali pakilo = kirai kielezi

Bo kakali = kirai kihusishi

Pakilo = kirai kielezi.

4.3.5 Kirai Kihusishi (KH)

Kirai kihusishi cha Kinyakyusa kinaweza kuwa neno moja au kundi la maneno ambacho neno lake kuu ni kihusishi. Kihusishi huweza kujalizwa na KN, KT au KE na huwa ni sehemu ya kundi kitenzi ambacho hufanya kazi kama vielezi. Endapo kirai kihusishi hiki cha Kinyakyusa kitajiri kama kiambajengo cha KN basi hutekeleza wajibu kama kivumishi (kwa mfano: umwana wa tata). Hivyo, kirai kihusishi hutumika katika kuifafanua nomino sawa na kifanyavyo kivumishi na huweza kutokea popote katika sentensi, kwa mfano:

i) Mwanzoni mwa sentensi

Pamwanya pa misi - juu ya maji

Kichwa cha kihusishi ni *pamwanya pa*.

ii) Mwishoni mwa sentensi

Fyosa itole fyapeleligwe *mu* mnyake na inongwa jwake - vyote vilifanyika

kwa huyo na neno lake..

Kichwa cha kihusishi katika sentensi (ii) ni *mu*.

4.3.5.1 Aina za Virai Husishi vya Kinyakyusa

Virai hivi vimegawanyika katika aina zifuatazo:

Vihusishi ya Mahali

Vihusishi hivi huonyesha mahali kwa mfano; *pambali pa* (kando ya), *pasi pa* (chini ya), *pamwanya pa* (Juu ya) na *pakati pa* (katikati ya), Mfano katika tungo virai vifuatavyo:

- i) Umundu atungesye *pasi pa* umpiki - mtu amekaa chini ya mti.
- ii) Imbene ilambalile *pambali pa* munngunda – mbuzi amelala pembeni ya bustani.
- iii) Imbeba jalingile *nkati mbwina* - Panya aliingia ndani ya shimo
- iv) *Nkyeni mu* myumba jake - mbele ya nyumba yake
- v) Atugesye *kifuki nu* moto - aliketi karibu ya moto

Vihusishi vya Wakati

Hivi ni vihusishi vinavyoonyesha wakati vinapotumika katika tungo. Navyo ni; *bo pakati* (kabla ya), *bo pakindile* (baada ya), *mpaka/ hadi* (mpaka), *ukufuma* (tangu).

Mfano katika tungo zifuatazo:

- i) *Ukufuma* nulubhunju bhalindikisye – tangu asubuhi wanasubiria
- ii) Bhafikile *bo pakali* akabalilo – walifika kabla ya muda
- iii) *Bo pakali* gwitu bhasokile - kabla ya yetu waliondoka

Vihusishi vya Sababu

Vihusishi hivi hutumika kuonyesha sababu inayopelekea jambo fulani kufanyika. Navyo ni; *ku nongwa ja* (kwa sababu ya) na *ku nogwa na isi* (kwa ajili ya hayo) sababu, Tungo kirai zifuatazo zinaonyesha namna vihusishi hivyo vinavyotumika.

- i) Bhampele igari *ku nongwa gwitu* - walimpa gari *kwa sababu yetu*
- ii) Ukwisa *ku nongwa na isi* - unakuja *kwa ajili ya haya*.
- iii) *Ku nogwa gwako nimpele* - *kwa ajili yako nimempka*

Vihusishi vya a-

Vihusishi hivi ni kama vile: gwa (kwa). Ja/pa (ya) , bwa, lwa (wa), ifya/sya (za); navyo vinaweza kutumika kama ifuatavyo:

- i) Ajobile inongwa *ja Kyala* – aliongea neno la Mungu
- ii) Umwana afikile *gwa Unkulumba jake* – mtoto alifika *kwa kaka/dada yake*
- iii) Fideo *ifya kubosya* - video vya kubonyeza
- iv) Na amalundi alyendile - *kwa miguu alitembea*
- v) Ikisu kya Tanzania - *nchi ya Tanzania*

4.3.5.2 Miundo ya Kirai Husishi cha Kinyakyusa

Kirai kihusishi ni neno linalohusisha mahusiano ya nomino na kile kinachotendwa katika tungo. Kirahi hiki cha kinyakyusa hujitokeza katika miundo tofauti kama ifuatavyo:

Kihusishi na kielezi (KH+E). Kwa mfano:

Injila ja *pamwanya* - njia ya juu

Ja = kihusishi

Kielezi = pamwanya

Ali pala ukufuma nulubhunju - alikuwa pale tangu asubuhi

Ukufuma = kihusishi

Nulubhunju = kielezi

Bakulyimbile mpaka isaa inu - wanaimba hadi saa hizi

Mpaka = kihusishi

Isaa inu = kielezi

Kihusishi na Nomino / Kiwakilishi.

Katika kirahi hiki neno kuu ni kihusishi kikiambatana na nomino ama kiwakilishi

chake. Kwa mfano aktika virai vifuatavyo:

Kalata gwa Kiswahili - kitabu cha Kiswahili.

gwa = kihusishi

Kiswahili = nomino.

Nkyeni mu myumba - mbele ya nyumba

Nkyeni mu = kihusishi

Myumba = nomino

Nkati pa mbwina - ndani ya shimo

Nkati pa = kihusishi

Mbwina = nomino

Kifuki ni une - karibu na mimi

Kifuki ni = kihusishi

Une - kiwakilishi

Kihusishi na kishazi kijalizi.

Bhafikile ukufuma panamajolo isaa moja nulubhunju - walifika tangu jana saa moja asubuhi.

Ukufuma - kihusishi

Panamajolo isaa moja nulubhunju - kishazi kijalizi

Juma akabuja *ukufuma* ulu asokilepo pakaja - Juma ajarudi tangu aondoke nyumbani.

Ukufuma - kihusishi

Ulu sokilepo pakaja - kishazi kijalizi

Tansania jakabile ubuhuru *ukufuma* ikyinja kya 1961 - Tanzania ilipata uhuru tangu mwaka 1961.

Ukufuma - kihusishi
 Ikyinja kya 1961 - kishazi kijalizi

Inyumba jijengigwe *pamoja pa* kyamba kintali Meru - nyumba imejenga juu ya
 mlima mrefu Meru.
 Pamoja pa - kihusishi
 Kyamba kintali Meru - kishazi kijalizi

4.4 Kuchanganua Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT) vya Kinyakyusa - Mtazamo wa X-baa

Uchanganua wa kirai cha lugha yoyote kwa kutumia nadharia ya X-baa ni kukigawa kirai kwa kuzingatia mahusiano baina ya neno kuu (kichwa) na vipengele vingine vinavyounda kirai hicho, ambapo kifundo hugawika katika matawi mawili pekee. Hivi ni kusema kuwa KN hakiwezi kuzalisha matawi matatu.

Radford (kishatajwa) anasema kuwa, kuna viwango vitatu vya kuchanganua virai navyo ni:

- i) Kategoria ya kiwango cha neno.

N = Nomino

T = kitenzi

V = kivumishi

H = kihusishi

E = kielezi.

- ii) Kategoria ya kiwango cha kati. Kwa mfano:

N = Nomino baa moja

T = kitenzi baa moja

V = kivumishi baa moja

H = kihusishi baa moja

E = kielezi baa moja

iii) Kategoria ya kiwango cha kirai kwa mfano;

KN = kirai nomino = N''

KT = kirai kitenzi = T''

KV = kirai kivumishi = V''

KH = kirai kihusishi = H''

KE = kirai kielezi = E''

ategoria za kati huwa kubwa kuliko kategoria kileksika lakini ndogo kuliko kategoria kamili yaani kirai kikuu. Maelezo ya mtaalamu huyo yametumika katika utafiti huu kama dira katika kuchanganua kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa kwa kuzingatia viwango vitatu vya uchanganuzi wa kirai kwa mtazamo wa X-baa.

Katika utafiti huu alama saidizi ya X' imetumika katika kuchanganua kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa kwa kuzingatia muundo wake. Ingawa wataalamu mbalimbali wamejaribu kuchanganua kirai kwa kutumia alama saidizi tofauti, kwa mfano, Radford (kishatajwa) alitumia alama saidizi ya X' na Chomsky alitumia alama saidizi ya \bar{X} na Jackendoff (kishatajwa) anatumia X kuwakilisha neno kuu (kichwa). Njia hizi tatu ni tofauti lakini zinaeleza jambo moja. Uchanganuzi wa kirai hiki umefanyika kwa kuzingatia miundo na aina za kirai kama ifuatavyo:

4.4.1 Kirai Nomino


Ni Kirai ambacho muundo wake umejikita kwenye nomino au mahusiano maalumu baina ya nomino na neno au mafungu ya maneno mengine. Radford (kishatajwa) kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai husika na uhainishwa kimuundo kulingana na neno kuu husika. Kwa mfano kirai ambacho neno kuu ni nomino au kiwakilishi huitwa kirai nomino. Uanishaji huu wa virai kimuundo hutegemea neno kuu katika kirai hicho. Kirai nomino hiki cha Kinyakyusa hujitokeza katika miuundo ifuatayo:

Nomino Pekee (N)

Ni kirai kinachoundwa na nomino pekee au Kiwakilishi chake. Kwa mfano:

- bhosa bhantali fijo – mti mrefu sana
- Jula unkulumba - yule mkubwa
- Imienda minyali - nguo chafu
- Amisi matalalifu - maji baridi
- Ikibusu kibofu - choo kibovu

Virai hizi zinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:







Mifano ya hapo juu inaonesha ambavyo kirai nomino pekee cha kinyakyusa au kiwakilishi chake kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Nomino na Kivumishi au kiwakilishi chake (N/W+V)

Katika tungo kirai hiki neno kuu linaweza kuwa nomino au kiwakilishi chake, kinajengwa kwa mahusiano baina ya neno kuu na kifungu cha maneno mengine. kwa mfano:

- Umkota umkangale ajobile – mzee mkubwa amesema
- Jula unkulumba - yule mkubwa darasani
- Ummanyisi mololo - mwalimu mpole
- Ikikota kibofu - kiti kibovu
- Pala po pamyabo pa nunu - pale kwao pa zuri

Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miuundo wake:







Kitenzi nomino na kivumishi (kitenzi nomino +V)

Ni muundo wa kirai unaojitokeza katika kirai nomino cha Kinyakyusa katika umbo la kitenzi ambacho kimeambikwa kiambishi awali “U” hali hii hufanya nomino hiyo kufanana sana na kitenzi. kwa mfano:

- Ukwimba pamyabo – kuimba kwao
- Ukwendile gwitu – kutembea kwetu
- Ukumanyisye Kiswahili mbombo ingafu- kufundisha Kiswahili kazi ngum
- Usyiganile kanunu - kupenda kuzuri

Nomino hizo zimeundwa kwa kunominisha kitenzi *kwimba*, *ikwenda*, *umanyisye* na *syiganile*. Virai hizi vinachanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miundo yake:







Nomino na Nomino (N+N)

Ni muundo mwingine pia unaojitokeza katika kirai nomino cha Kinyakusa. Kirai hiki huundwa kwa nomino mbili. Nomino ya kwanza ndio chimbuko la mahusiano yaliyopo na maneno mengine yanayounda kirai hicho. kwa mfano:

- Ikyindi gwa imbene – ungali na mbuzi
- Unkota ni bhana - mzee na watoto
- Abakangale ni abakeke - wazee na vijana
- Ikyai ni kisyesye - chai na mkate
- Alilye ikyindi ni nguku - alikula wali na kuku

Virai hiki kinaweza kinachanganuliwa kama ifuatavyo:







Katika mifano ya sentensi hapo juu, nomino za kwanza ndiyo chimbuko la mahusiano kati yake na maneno mengine.

Nomino na Kivumishi na Kivumishi (N+V+V)

Ni muundo wa kirai nomino unaojengwa kwa kuzingatia mahusiano kati ya neno kuu yaani, nomino na virai kivumishi. Kwa mfano:

- Jula mnini fiyo – yule mdogo sana
- Ugwe mmanyani nkamo fiyo– wewe rafiki mjanja mno.
- Igorofa lyelu itali - gorofa jeupe refu
- Ummanyisi John nkali fujo - mwalimu John nkali sana
- Ikijiji inywamu ukukinda ikisu - kijiji kikubwa zaidi nchini







Nomino na Kivumishi na Kielezi (N+V+E)

Ni kirai ambacho huundwa na nomino au kiwakilishi chake. Neno chimbuko la mahusiano baina ya maneno mengine katika kirai hicho ni nomino. kwa mfano:

- Ibegi sito ukukinda – begi zito zaidi
- Jula mnunu fiyo – yule mzuri sana
- Omwana nandi fiyo - mtoto mdogo mno
- Irangi nditu fiyo - rangi nyeusi sana
- Ijiko ibofu kangi - jiko bovu tena

Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia miundo yake kama ifuatavyo:







Mifano ya sentensi hapo juu, nomino ndiyo neno kuu linalounda virai hivyo.

Nomino na Kihusishi (N+KH)

Ni aina nyingine ya muundo kirai ambacho hujitokeza katika kirai nomino cha Kinyakyusa. huundwa kwa kuzingatia mahusiano maalumu baina ya neno kuu nomino na kirai kihusishi. Kwa mfano:

- Omwana gwa tata – mtoto wa baba
- Umpiki gwa bumi – mti wa uzima
- Roza mpaka lilino akalipo - Roza mpaka leo yupo
- Ilisyu kya Bumi - neno la uzima

Virai hivi navyo vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miundo yake:




Miundo ya virai hapo juu inaonyesha namna virai hivyo vya Kinyakyusa vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia mahusiano yake baina ya kichwa KN

na KH katika kukijenga. Vile vile kirai nomino hiki kinaweza kuundwa kwa kutanguliwa na kihusishi kama kifungu cha maneno kinachoambatana na nomino.

Kwa mfano :

- pa misi alambalike – kwenye maji amelala.
- Bo pakali ugwe kusoka - kabla ya wewe kuondoka

Miundo hii ya kirai vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:



Mifano hiyo inatuonyesha namna ambavyo kirai nomino cha Kinyakyusa kinavyoweza kujengwa kwa kutanguliwa na KH na kisha kufuatiwa na KN na pia huweza kuchanganuliwa kwa kufuata muundo wake.


Nomino na Kishazi tegemezi (N+KTg)

Huu pia muundo unajitokeza katika kirai nomino cha Kinyakyusa, ambapo neno chimbuko la mahusiano ni nomino inayoambatana na kishazi tengemenzi kinachotaliwa na kitenzi kisichojitosheleza kima. Kwa mfano katika virai nomino vifuatavyo:

- Umwana ujugwalimbene jo mwanangu – mtoto uliyemwona ni wakwangu

- Ifula jotimile pakilo jalionangile ululalo – mvua iliyonyesha usiku iliharibu daraja.
- Umyambala ujauwegile Janeth unkali - mwanaume aliyemwoa Janeth mkali
- Igari ililigwile mmajolo lisosigwepo - gari lililoanguka jana limeondolewa
- Umundu gwegwesa isege kilabo - mtu yeyote aje kesho

Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miundo yake:




Mifano ya sentensi hapo juu, inatuonyesha virai nomino vinavyoundwa na neno kuu KN na vishazi tengemezi. Vishazi tegemezi ni vishazi ambavyo ndani yake huwa na o-rejeshi. Mfano “**ililigwile**” ‘li’ inawaonyesha urejeshi ikiirejelea nomino igari.

Nomino na Kibainishi (N+Kib)

Ni muundo mwingine ambao pia hujitokeza katika kirai cha Kinyakyusa ambapo huundwa na nomino kama neno kuu likiambatana na kibainishi ambacho ufanya kazi ya kuibainisha nomino inayotajwa katika kirai hicho. Kwa mfano:

- Jula unkikulu - yule mwanamke
- Iki Ikitabu – hiki kitabu
- Uju Kyala gwitu - huyu Mungu wetu
- kila ikijiji - hiki kijiji
- Juma yule nsomari - yule Juma msomari

Virai hizi vinaweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia miundo yake kama ifuatavyo:





Katika mifano ya virai hapo juu, kibainishi kimetumika katika kuibainisha nomino inayotajwa. Haegeman (kishatajwa) Hadhi ya juu ya kirai inapatikana kwa kuunganisha X' ya juu kabisa na kibainishi ili kuunda ufasiri wa juu kabisa wa X'.


Kibainishi na Nomimo na Kivumishi (Kib+N+V)

Huu ni muundo mwingine pia unaojitokeza katika kirai nomino cha Kinyakyusa. Licha ya kuwepo kwa muundo wa kirai nomino + kibainishi katika kirai cha Kinyakyusa, pia kirai hicho kinaweza kujitokeza katika muundo wa Kib + Nomino + Kivumishi ambapo kibainishi kimetumika kudhihirisha upekee wa nomino. kwa mfano:

- Jula unkikulu untengamojo fijo pala pa kijiji – yule mwanamke mnyenyekevu sana pale kijijini.
- Loveness Jo undendwana nnunu pa kijiji – Loveness ndiye msichanana mzuri pale kijijini.
- Uju Unkikulu nkangafu itolo - yule msichana mkali sana
- Iki ikijiji kinandi - hiki kijiji kidogo

Miundo hii ya virai hunaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:





Katika mifano ya virai hapo juu vibainishi vimetumika katika kuibainisha nomino inayotajwa katika tungo zilizochanganuliwa hapo juu.

4.4.2 Kirai Kitenzi (T)

Matei (kishatajwa) kirai ni fungu la maneno ambalo hufanya kazi kama neno moja au huwa na uamilifu sawa. Hivyo kirai ni fungu la maneno ambalo huundwa na neno moja au zaidi. Maelezo ya mtaalamu huyo yalisaidia katika kukibaini Kirai kitenzi cha Kinyakyusa na kuwezesha kukichanganua. Kirai hiki cha Kinyakyusa huweza kuwa neno au fungu la maneno.ambalo huwa ni kichwa cha kirai. Kirai kitenzi hiki huweza kuwa pekee au kikifuatwa na kijalizo hasa katika vitenzi vishirikishi. Kitenzi hiki hujitokeza katika aina tatu ambazo ni kitenzi kikuu, kitenzi visaidizi na kitenzi kishirikishi. Vitenzi hivi huweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia miundo yake kama ifuatavyo:

4.4.2.1 Kitenzi Kikuu (T)


Katika kirai kitenzi hiki neno kuu linalotawala huwa ni kitenzi kikuu. Nacho hujitokeza katika miundo ifuatayo:

Kitenzi Kikuu Pekee (T)

Ni kirai kinachoundwa na kitenzi kikuu pekee. Neno kuu katika kirai hiki ni kitenzi kikuu. Kwa mfano:

- Ukwenda kusukulu – kwenda shuleni
- Kutusya panandi – kupumzika kidogo
- Katele - choka
- Ajobile - amesema

Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:




Katika uchanganuzi wa hapo juu, alama T' inawakilisha kichwa cha kirai kitenzi hicho kinachounda kirai kitenzi pekee.

Kitenzi na Nomino / Kiwakilishi (T+N/W)

Ni pia ni kirai ambacho neno kuu ni kitenzi kikuu ambacho ndiyo chimbuko la mahusiano yaliopo katika maneno yanahusika katika kirai hicho. Kwa mfano:

- Twalimmwambilike umwana gwako - tulimpokea mtoto wako
- Tukwaganile bhosa paitasi – tunakutana wote baadaye
- Syonangike isyene - zimeharibika zenyewe
- Atugesye ikikota kinyali - amekalia kiti kichafu





Miundo ya virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:



Kirai hiki pia kinaweza kuundwa kwa kutanguliwa na kirai nomino au Kiwakilishi chake na kufuatiwa na kichwa. Kwa mfano katika tungo:

- Uhiji atesigwe fijo – mwizi aliadhibiwa mno
- Jula akwisa - yule anakuja.
- Isyene syonangike - zenyewe zimeharibika
- Kila kisobile kangi - kile kimepotea tena

Virai hivi vinachanganuliwa kama ifuatavyo:







Kitenzi kikuu na Nomino na Kirai kivumishi (T+N+V)

Ni aina nyingine ya muundo wa kirai kitenzi unaojitokeza katika kirai kitenzi kikuu cha Kinyakyusa. Katika kirai hicho neno kuu ni kitenzi kikuu kinachoundwa kwa kuzingatia mahusiano yake na virai vingine. Kwa mfano:

- Tata gwitu atwale igari inywamu – baba yetu ameleta gari kubwa
- Bhasokilepo abhasukulu bhosa kusukulu - Wameondoka wanafunzi wote shuleni
- Nulile isyati lyelu mwiluka - nimenunua shati leupe dukani
- Jikutilisya ingisi sito - linatisha giza nene

Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miundo yake:







Kitenzi kikuu na Nomino na Kielezi (T+N+E)

Pia kirai kitenzi kikuu cha Kinyakyusa huwa na muundo wa T+N+E. Neno kuu katika kitenzi hiki ni kitenzi kikuu. Kwa mfano:

- John Ikulonda imbombo kumbwani = John anatafuta kazi mjini
- Nalile isyati mmajolo = nimenunua shati jana

- Ulukamano lwabombigwe Chato isaa sita pamusi = mkutano ulifanyika Chato saa sita mchanna
- Wahesya bhalilemo ivindu pakilo = wageni walikula chakula usiku

Virai hivii vinaweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia miundo yake kama ifuatavyo:




Kitenzi kikuu na kielezi (T+E)

Ni muundo mwingine wa kirai unaojitokeza katika kirai kitenzi cha Kinyakyusa, ambapo neno kuu ni kitenzi kikuu kikiambatana na kielezi au kirai kielezi katika kukiunda. Kwa mfano:

- Bhalimbwene kukaja gwitu mmajolo – walimwona nyumbani kwetu jana..
- Tukwaganile kabili kabili - tunakutana mara kwa mara
- Ungala bwalwa endaga ikubelabela - mlevi anatembea akipepesuka
- Alyemdile na malundi - alitembea kwa miguu




Virai viki vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia muundo wake:



Kirai kitenzi hiki pia kinawenza kujitokeza kikiwa kimetanguliwa na kielezi. Kwa mfano katika virai kitenzi hivi:

- Nulubhunju bhasokile - asubuhi na mapema waliondoka
- Kangi babujile - tena walirudi
- Fijo balabile - mapema walifika

Navyo vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:







Kitenzi kuu na Vielezi Viwili (T+E+E)

Ni muundo mwingine pia unaojitokeza katika kirai kitenzi kikuu cha Kinyakyusa. Kitenzi hicho ndiyo chimbuko la mahusiano baina yake na virai vingine. Kwa mfano:

- Ummage umugi gusobile kukaja lilinu – kisu kikali kimepotea nyumbani leo
- Imbimbibi asokile mkipanga – Haraka aliondoka kanisani
- Bhosa balyimbile kanunu fijo = wote waliimba vizuri sana
- Jula tukwaganile kabili kabili kuimbombo = yeye tunaonana mara kwa mara kazini
- babujile kangu kukaja = walirudi tena nyumbani

Vira hivi navyo vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miundo yake.



Kitenzi kikuu na Kirai kihusishi na Nomino (T+KH+N)





Ni muundo mwingine tena unaojitokeza katika kirai kitenzi kikuu cha Kinyakyusa.

Neno kuu linalotawala ni kitenzi kikuu. Kinaundwa kwa kuzingatia mahusiano maalumu baina yake na virai vingine. Kwa mfano:

- Inyumba jjjengigwe kifuki ni nyanja - nyumba imejengwa karibu na ziwa
- Asokilepo kisita ulusa – aliondoka bila ruhusa

- Unkota atugesye pasi pa umpki = mzee ameketi chini ya mti
- Aisha alinganile kunongwa ja ubupe = alimpenda kwa sababu ya mali
- Afikile bo kikindile ikimogo = alifika baada ya sherehe




Virai vitenzi hiki vinachanganuliwa kwa kuzingatia miuundo yake kama ifuatavyo:



Kirai hiki pia kinaweza kujitokeza katika muundo wa T+N+KH+N. kama ifuatavyo:

- Inguku jitetile amafumbi pasi pa mpiki = kuku ametanga mayai chini ya mti
- Ajobile inongwa jo Kyala = ameongea neno la Mungu

- Nkunganile ikisu kya Tanzania = naipenda nchi ya Tanzania





Kitenzi Kikuu na Kirai husishi na Kivumishi (T+KH+KV)

Pia kirai kitenzi kikuu hii cha Kinyakyusa kinaweza kujitokeza katika muundo huu wa T+KH+KV ambapo T ndiyo chimbuko la mahusiano baina ya mafungu mengine ya maneno. Mfano katika sentensi zifuatazo:

- Juma asekile nkyeni mu jake = Juma alicheka mbele yake
- Kiyendile mu lukani = kilienda kwa ubishi
- Po ajobile jo mmyake = aliongea ya kwake tu
- Imbene ilambalike pambali pa mmyake = mbuzi alilala mbeni yake





Virai vitenzi hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia muundo wake.



Kitenzi kikuu na Kirai Kihusishi na Kielezi (T+KH+KE)

Pia vile vile kirai kitenzi kikuu hiki kinaweza kujitokeza kikiandamana na kirai kihusishi ambacho pia kikifuatiwa na kirai kielezi katika kukikamilisha kirai hicho. mfano katika sentensi zifuatazo:

- Ambonile pabhutali fiyo = alimwona kwa mbali sana
- Aneth asokapo ukufuma mmajolo = Aneth aliondoka tangu jana
- Nndipo mpaka pakilabo nulubhunju = nitakuwepo hadi kesho asubuhi
- Walindikisye ukufuma mmajolo = wamesuburi toka/tangu jana







4.4.2.2 Kitenzi Kisaidizi na Kitenzi Kikuu (Ts+T)

Kitenzi kisaidizi cha Kinyakyusa, ni kitenzi ambacho kinaandamana na kitenzi kikuu hasa pale ambapo kitenzi husika kinahusisha hali. Kitenzi hiki kinaweza kuwa kitenzi kimoja au viwili zinavyotangulia kitenzi kikuu. Hivyo basi kirai hiki uhusisha vitenzi viwili katika kukijenga. Kwa mfano:

Kitenzi Kisaidizi na Kitenzi kikuu Kimoja (Ts+T)





- Ugwe jo ukwimba = wewe ulikuwa unaimba
- bhafikile babujile kangi = walifika wakarudi tena
- bhosa bhasokilepo atwelepo igari = wote waliondoka alipoleta gari
- Ulwisi jo lwaliswile amatope = mto ulikuwa umejaa matope.
- Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:



Vitenzi Visaidizi viwili na Kitenzi Kikuu (Ts+Ts+T)

- Ingisi jo jikutilisya kujatya pakilo - giza lilikuwa linatisha kutembea usiku
- Juma ali kubhuka kuipuita mu kipanga - Juma alikuwa anakwenda kuomba kanisani.
- Alilemo akasokapo kubhuka ulukomano - alikula akaondoka kwenda mkutanoni
- Akabangale gitu bhali bhakafika kutuponya - wazee wetu walikuwa hajafika kutuona

Virai hivi navyo vinaweza kuchanguliwa kama ifuatavyo kwa kuzingatia miundo yake.



Katika mifano ya hapo juu, inatuonyesha vitenzi visaidizi viwili ambavyo vimekitangulia kitenzi kikuu ili kukamilisha taarifa iliyokusudiwa. Kwa mfano “bhali bhakafika – walikuwa hajafika” tungo hii inaleta maswali kama vile ‘wapi?, kwanini? Na kufanya nini?

4.4.2.3 Kitenzi Kishirikishi


Kitenzi kishirikishi cha Kinyakyusa ni kirai ambacho huhitaji kijalizo ili kiwe kikamilifu. Kinahitaji vijalizo ambavyo vinaweza kuwa nomino, kielezi ama kivumishi. Kirai hiki hujitokeza katika miundo ifuatavyo:


Kitenzi kishirikishi na Nomino (t+KN)

Ni muundo wa kirai ambao huundwa kwa kuzingatia mahusiano baina ya neno kuu yaani kitenzi kishirikishi na kirai nomino. Kwa mfano katika virai vitenzi vifuatavyo:

- Umwene jo Kyalaa gwitu – Yeye ndiye Mungu wetu
- Johani ni gwasukulu ugwamaka fijo – Johani ni mwanafunzi hodari sana
- Aligwa sukulu - alikuwa mwanafunzi
- Julia ni uhiji - yule ni mwizi

Virai hivi vinaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:







Kitenzi kishirikishi na Kielezi (t+KE)

Pia ni Muundo wa kirai unaojitokeza katika kirai kitenzi kishirikishi cha Kinyakusa. Neno kuu katika kirai hiki ni kitenzi kishirikishi. Kirai hiki huundwa kwa kuzingatia mahusiano maaluma baina yake na kirai kielezi katika kukikamilisha. Kwa mfano katika virai kitenzi vishirikishi vifuatavyo:

- Damas jo pachipatala - Damas alikuwa hospitalini
- Pala po pakaja kumyake – pale ndipo nyumbani kwake
- Ikibutu jali nkati - choo kilikuwa ndani
- Pala po pakaja = pale ndipo nyumbani

Miundo ya virai hizi inaweza kuchanganuliwa kama ifuatavyo:







Kitenzi kishirikishi na Kirai vumishi (t+KV)

Ni muundo mwingine tena unaojitokeza katika kirai kitenzi kishirikishi cha Kinyakyusa. Neno linalotawala katika kirai hiki ni kitenzi kishirikishi kinachoambatana na kirai vumishi kinachofanya kazi ya kijalizo katika kukikamilisha. Kwa mfano:

- Julieth jo ntengamojo – Janeth ndiye mnyenyekevu
- Injoka jo Jakindilile - nyoka alikuwa mwelevu
- Ikikota kyali kinyali - kiti kilikuwa kichafu
- Isahani jali inyali - sahani ilikuwa chafu

Virai hivi vinachanganuliwa kwa kuzingatia miundo yake kama ifuatavyo:





4.5 Hitimisho

Katika uchambuzi wa data mtafiti ameweza kubainisha, kuchanganua na kuwasilisha virai vya Kinyakyusa kwa kufuatana na maswali yake ya utafiti.

Katika ubainishaji na uainishaji wa kirai cha Kinyakyusa mtafiti ameweza kupata miundo na aina mbalimbali ya virai vya Kinyakyusa. Aidha, mtafiti ameonyesha virai hivyo vya Kinyakyusa vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Matokeo hayo yamedhihirisha kuwa kirai cha Kinyakyusa kinaweza kubainishwa, kuainishwa na kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya X-baa kwa kuzingatia miundo yake.

SURA YA TANO

5.0 MATOKEO YA UTAFITI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu Uchanganuzi wa Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT) cha Kibantu – Mtazamo wa X-baa: Mfano Kutoka Virai vya Kinyakyusa. Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa sura yenyewe. Sehemu ya pili inahusu muhtasari wa utafiti na utafiti. Sehemu ya tatu inahusu matokeo ya utafiti. Sehemu ya nne inaelezea kuhusu mchango wa utafiti na Sehemu ya tano inahusu mapendekezo mbalimbalina.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu, ulilenga kuchanganua kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha kibantu kwa kutumia nadharia ya X-baa : Mfano virai vya Kinyakyusa. Utafiti huu hasa ulijitikita kuchunguza mambo makuu matatu. Kwanza, kubainisha virai vya Kinyakyusa. Pili, kuainisha virai hivyo kwa kuzingatia miundo yake. Tatu kuchanganua virai viwili yaani, kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Nadharia ya X-baa ilitumika katika uchanganuzi na kuonyesha namna virai vya Kinyakyusa vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia miundo yake. Kupitia nadharia hii imebainika namna virai vya lugha nyingine za kibantu vinavyoweza kuchanganuliwa kama ilivyochambuliwa katika Sura ya Nne.

Utafiti huu ulifanyika mkoani Mbeya katika wilaya ya Ipinga, kijiji cha Ipinda na kata ya Ipinda kwa sababu ni eneo ambalo mtafiti anauzoefu nalo. Jumla ya watafitiwa 10, wazawa wa lugha hiyo walisaidia kupata data ambazo zimetumika katika utafiti huu. Utafiti huu ulitumia mbinu za usaili na kushiriki katika mchakato wa kukusanya data.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umefanikiwa kubainisha virai vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa, kuvianisha virai hivyo kwa kuzingatia miundo na mahusiano yake baina ya neno kuu na maneno mengine katika kuvijenga, na pia kuvichanganua virai viwili yaani, kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) kwa kutumia nadharia ya X-baa ambayo bado haijafahamika kwa walio wengi katika taaluma hii ya Sintaksia ya Uchanganuzi wa Sentensi.

Utafiti umebaini kuwa nadharia ya X-baa inaweza kutumika katika kuchanganua virai vya lugha nyingine za kibantu kwa usahihi kabisa kwa kuzingatia miundo ya virai vya lugha husika.

5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu una mchango mkubwa kwani umeweza kubainisha aina za virai vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa na kuvianisha virai hivyo kwa kuzingatia miundo yake na mahusiano yaliyopo baina ya neno kuu na maneno mengine katika kuvijenga.

Sambamba na hilo utafiti huu umeweza kuchanganua virai viwili vya Kinyakyusa yaani, kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) kwa kutumia nadharia ya X-baa. Mchango huu ni msaada mkubwa kwa wanataaluma wa Sintaksia ya uchanganuzi wa sentensi kwani itawasaidia kupata maarifa mapya yanayohusu uchanganuzi wa sentensi za lugha nyingine za kibantu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa.

Idadi ya tafiti na maandiko yanayohusu uchanganuzi wa sentensi hasa sentensi za lugha nyingine za kibantu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa ni machache. Kazi hii, kwa hiyo imeongeza idadi ya tafiti na maandiko ambayo yatatumika kama marejeleo kwa wasomi wajao.

5.5 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo

Utafiti huu umejishughulisha na ubainishaji, uanishaji na uchanganuzi wa virai viwili yaani kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) cha Kinyakyusa. Kutokana na muda na malengo ya utafiti, utafiti haukuweza kuchanganua virai vingine vya Kinyakyusa na kushughulikia aina nyingine za tungo zilizomo katika lugha hiyo. Mtafiti anapendekeza watafiti wengine wa taaluma ya Sintaksia ya Uchanganuzi wa sentensi (tungo) kufanya utafiti katika tungo nyingine na tungo ambazo utafiti huu haukugusia kama vile uchanganuzi wa sentensi, vishazi na kijalizo cha Kinyakyusa. Pia mtafiti anapendekeza utafiti ufanyike katika virai vya lugha nyingine za kibantu ambazo havijaweza fanyiwa utafiti huu, ili kuweza kubainisha, kuainisha na kuchanganua virai hivyo kwa kutumia nadharia ya X-baa.

5.6 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa muhtasari utafiti unaohusu “Uchanganuzi wa Kirai nomino na Kirai tenzi cha Kinyakyusa kwa kutumia nadharia ya X-baa” . katika sura hii mtafiti ameeleza malengo ya utafiti, mbinu alizotumia kukusanya data, eneo ambapo utafiti umefanyika pamoja na nadharia iliyotumika katika kuchanganua data. Aidha uchanbuzi wa data umeelezwa na matokeo ya utafiti yameelezwa kwa ufasaha. Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa nadharia ya X-baa inaweza kutumika katika kuchanganua virai vya lugha nyingine za kibantu kikiwemo Kinyakyusa kinachozungumzwa mkoani Mbeya kwa usahihi kabisa kwa kuzingatia miundo ya virai vya lugha hiyo. Aidha maeneo yanayohitaji utafiti zaidi yamebainishwa.

MAREJEO

- Adam, J. & Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies*. Mzumbe Book Project, Morogoro, Tanzania.
- Andrews, R. (2003). *Research Question (Continuum Research Methods)*. London: Bloomsbury Academic Press.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: MIT Press.
- Cowper, E. (1992). *A Concise Introduction to Syntactic Theory: The Government-Binding Approach*. Chicago: The University of Chicago Press.
- Culicover, P. (1976). *Syntax*. New York: Academic Press.
- Elali, A. (2012). *Kikundi Nomino cha Kiswahili kwa Kutumia Nadharia ya X-baa. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya*.
- Felberg, K. (1996). *Nyakyusa – English Swahili and English-Nyakyusa Dictionary*: Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publisher.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.
- Haegeman, L. (1991). *Introduction to Government and Binding Theory*. London: Blackwell Publishers.
- Jerono, P. (2003). *Kishazi huru Arifu cha Kiswahili: Mtazamo wa X-baa. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya*.
- Kihore, M. Y. na Wenzake (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu – Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kothari, C. H. (2003). *Research Methodology – Methods and Techniques (2nd Ed)*. New Delhi: New Age International Publishers.
- Kothari, C. H. (2008). *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.

- Kumar, K. (1996). *Reference Service*, (5thed). New Delh: Ravindra Offset Press.
- Longhorn, (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.
- Lusekelo, A. (2007). *Structure of the Nyakyusa Noun Phrase*: University of Dar es Salaam, College of Education, Dar es Salaam, Tanzania.
- Mabo, J. F. (1999). *A Comporative study of Bantu Noun classes*. Gottenbang: ACTA University Gothoburgensis Press.
- Mabo, S. M. & Sands T. G. (2002). *The Language of Tanzania: A Bibliography*. Gothenburg: ACTA Univesity Gothoburgensis Press.
- Massamba, D. P. na wenzake, (2008). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Falsafa na Isimu*. Dar es Salaam: TUKI
- Matei, A. (2008). *Sarufi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.
- Mbesa, N. (2008). Mofosintaksi ya Kishazi Nomino cha Kiswahili sanifu: Mtazamo wa X-baa. Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Mekacha, R. (2000). *Isimijamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.
- Nyaga, L. (2011). Mofosintaksi ya kishazi kielezi cha Kiswahili sanifu: Mtazamo wa X-baa. Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Olali, T. (1998). Kirai nomino cha Kiswahili: Mtazamo wa X-baa” Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Radford, A. (1988). *Transformational Grammar*: Cambridge: Cambridge University Press.
- Radford, A. (2004). *English Syntax: An introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Rubanza, Y. (2013). *Sarufi Mtazamo wa Kimuundo*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Istmu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

VIAMBATANISHO

Tungo kirai za Kinyakyusa zilizotumika katika utafiti huu.

Kinyakyusa

1. Kyala wa kumwanya
2. Umpiki untali
3. Jula unkota
4. Ukwimba pamyabo
5. Ikyindi gwa imbene
6. Igali inywamu fijo
7. Ugwasukulu mnini mmaganyi
8. Omwana gwa tata
9. Umwana ujugwalimbwene jo mwanangu
10. Jula unkikulu
11. Jula unkikulu untengamojo fijo
12. Ukwenda
13. Ugwe jo ukwimba?
14. Bhalimbwene kukaja
15. Twalimmwambilike umwana
16. Atwele imbene gwa mjomba
17. John atwale igari inywamu
18. Ikulonda imbombo inunu
19. Inyumba jijengigwe kifuki ni nyanja
20. Julieth jo umtengamojo
21. Injila intali jikukatasya
22. Umwana mmaganyi nkamu fijo kukaja
23. Bhabukile Iluka inywamu fijo kula kukijiji
24. Bhana bhosa bhabukile gwa mjomba
25. Unkangale umwene iluka inywamu kula
26. kukijiji afikile imbimbibi
27. Balabile nulubhunju
28. Unkikulu mnunu fijo
28. Imbene ilambalile ichumba pambali pa liliko
29. Pamwanya pa misi
30. Fyosa itole fyapeleligwe mu mnyake na Inongwa jwake
31. Kumpiki gwa bumi
32. Injila ikubuka pakati pa munngunda
33. Gwa mjomba kuntali fijo

Kiswahili

- Mungu wa mbinguni
 Mti mrefu
 Yule mzee
 Kuimba kwao.
 Ugali na mbuzi.
 Gari kubwa sana.
 Mwanafunzi mdogo mtundu
 Mtoto wa baba.
 Mtoto uliyemwona ndiye mwanangu
 Yule mwanamke.
 Yule mwanamke mwema sana
 Kutembea
 Wewe ndiye mwimbaji?
 Walimwona nyumbani
 Tulimpokea mtoto
 Alileta mbuzi kwa mjomba
 John alileta gari kubwa .
 Anatafuta kazi nzuri
 Anaishi karibu na ziwa
 Julieth ndiye mwema
 Safari ndefu inachosha
 Mtoto mtundu mjanja sana nyumbani
 Walitembelea duka kubwa sana kule kijijini
 Watoto wote walikwenda kwa mjomba
 Mzee mwenye duka kubwa kule kijijini
 alifika haraka.
 Waliwahi asubuhi
 Mwanamke mzuri sana
 Mbuzi alilala chumbani kando ya jiko.
 Juu ya maji
 Vyote vilifanyika kwa huyo na kwa neno lake
 Mti wa uzima
 Njia iendayo katikati ya bustani
 Kwa mjomba mbali sana.

- | | |
|--|---------------------------------------|
| 34. Umundu atusyege pasi pa umpiki | Mtu amekaa chini ya mti. |
| 35. Imbene ilambalile pambali pa munngunda | Mbuzi amelala pembeni ya bustani |
| 36. Ukufuma nulubhunju bhalindikisye | Tangu asubuhi wanasubiria |
| 37. Bhafikile bo pakali akabalilo | Walifika kabla ya muda |
| 38. Bhampele igari ku nongwa gitu | Walimpa gari kwa sababu yetu |
| 39. Ukwisa ku nongwa na isi! | Unakuja kwa ajili ya haya!. |
| 40. Ajobile inongwa ja Kyala | Aliongea neno la Mungu |
| 41. Umwana afikile gwa Unkulumba jake | Mtoto alifika kwa dada (mkubwa) yake. |
| 42. Fideo ifya kubosya | Video vya kubonyeza. |
| 43. Injila ja pamwanya | Njia ya juu |
| 44. Kalata gwa Kiswahili | Kitabu cha Kiswahili. |
| 45. Bhafikile ukufuma nulubhunju | Walifika tangu asubuhi. |
| 46. Ajobile kanunu | Ameongea vizuri |
| 47. Bhosa Bhasokile kubuka kukipanga | Wote waliondoka kwenda kanisani |
| 48. Bandu bhosa bhasokile | Watu wote waliondoka |
| 49. Imbene jibhatigwe lilino nulughunju | Mbuzi amejichwa leo asubuhi |
| 50. Umbulile uju ungwakumwaga pakaja | Mwambie utakayemkuta nyumbani |
| 51. Alinkwalamila pamwanya pamisi | Alitulia juu ya maji |
| 52. Nulubhunju bhasokile | Mapema waliondoka |
| 53. Umwene jo Kyala | Yeye ndiye Mungu |
| 54. Jo Kyala gitu | Ndiye Mungu wetu |
| 55. Damas jo jakindilile fijo | Damas alikuwa mwerevu sana |
| 56. Umundu atungesye pasi pa umpiki | Mtu amekaa chini ya mti |
| 57. Imbene ilambalile pambali pa mumngunda | Mbuzi amelala pembeni ya bustani |
| 58. Bhampele igari ku nongwa gitu | Walimpa gari kwa sababu yetu |
| 59. Ukufuma nulighunju bhalidnisye | Tangu asubuhi wanasubiria |
| 60. Pasi pa umpiki | Chini ya mti |
| 61. Pakati pa mumngunda | Katikati/ ndani ya bustani |
| 62. Bhafikile bo pakali akabalilo | Walifika kabla ya muda |
| 63. Jijengigwe kifuki ni njanya | Imejengwa karibu na ziwa |
| 64. Ajobile inongwa ja Kyala | Aliongea neo la Mungu |
| 65. Fideo ifya kubosya | Video ya kubonyeza |
| 66. Ukwisa ku nongwa na isi? | Unakuja kwa ajili ya haya? |
| 67. Uhiji atasigwe fijo | Mwizi ameadhibiwa mno |
| 68. Jula akwisa | Yule anakuja |
| 69. Bhalimbwene kukaja gwiti mmajolo | Walimwona nyumbani kwetu jana |
| 70. Tukwaganile kabili kabili | Tunaonana mara kwa mara |
| 71. Kangi babujile kukaja | Tena wamerufi nyumbani |
| 72. Nalile isyati mmajolo | Nilinunua shati jana |
| 73. Bhasokile abhosukulu bosa kusukulu | Wameondoka wanafunzi wote shuleni |

74. Ummage umngi gusobile kukaja lilino
Kisu kikali kimepotea nyumbani Leo.
75. Imbimbibi asokle mkipanga
Haraka haraka aliondoka Kanisani.
76. Asokilepo kisita ulusa
Aliondoka bile ruhusa
77. Damas jo pachpatala
Damas alikuwa hospitalini
78. Pala po pakaja kumyake
Pale ndipo nyumbani kwake
79. Juba ikulonda ukususya
Mama anataka kupumzika
80. Neema jo ikumanyisye bhana
Neema alikuwa anafundisha watoto
81. Aukubuja kilabho
Atarudi kesho
82. Lilino nulubhunju basokile
Leo hii asubuhi waliondoka
83. Nulubhunju bo pakali akubhalilo afikile
Asubuhi na mapema kabla ya muda alifika
84. Walindikisye ukufuma mmajolo pakilo
Wamesubiri toka / tangu jana jioni
85. Umwana unyambala apapigwe
Mtoto wa kiume amezaliwa
86. Imbene nnini jasobhile mmajolo bo jibhonike
Mbuzi mdogo aliyepotea jana amepatikana
87. Asokile ukufuma mmajolo
Ameondoka tangu jana
88. Bhafikile bo pakindile unkota kusoka
Walifika baada ya mzee kuondoka
89. Unkota umkangale ajobile
Mzee mkubwa kiumri amesema
90. Jula unkulumba fijo
Jule ni mkubwa
91. Ukwendile gwitu
kutembea kwetu
92. Ugwe mmanyi nkamo fijo
Wewe rafiki mjanja sana
93. Bo pakali ugwe kusoka
Kabla yaw ewe kuondoka
94. Ifula jotimile pakilo jalionangile ululalo
Mvua iliyonyesha usiku imeharibu daraja
94. Jula unkikulu nkangafu itolo
Yule mwanamke mkali sana
95. Loveness jo undendwana nnunu pa kijiji
Loveness ndiye msichana mzuri pale kijijini
96. Kutusya panandi
Kupumzika kidogo
97. Tukwaganile bhosa paitasi
Tutaonana wote baadaye
98. Umundu gwegwesa isege kilabu
Mtu yeyote aje kesho
99. Iki ikijiji kinandi
Hiki kijiji kidogo
100. Kila kisobile kangi
Kile kimepotea tena
101. Nnulile isyati lyelu mwiluka
Nimenunua shati jeupe dukani
102. Jikutilisye ingisi sito
Linatisha giza nene
103. Ulukamano lwabambigwe Chato isaa sita Pamusi
Mkutano ulifanyka Chato saa sita mchana
104. Wahesya bhalilemo ivindu pakilo
Wageni walikula chakula usiku
105. Ungala bwalwa endaga ikubelbela
Mlevi anatembea akipepesuka
106. Alyendile na malundi
Alikwenda kwa miguu
107. Afikile bo kukindile ikimogo
Alifaika baada ya sherehe

- | | |
|---|------------------------------------|
| 109. Inguku jitetile amafumbi pasi pa mpiki | Kuku ametanga mayai chini ya Mti. |
| 110. Nkunganile ikisu kya Tanzania | Naipenda nchi ya Tanzania |
| 111. Juma asekile nkyeni mu jake | Juma alicheka mbele yake |
| 112. Po ajobile mmyake | Aliongea yak wake tu |
| 113. Nndipo mpaka pakilabo | Nitakuwepo hadi kesho |
| 114. Ulwisi jo lwaliswile amatope | Mto ulikuwa umejaa matope |
| 115. Ingisi jo jikutilisya kyatya pakilo | Giza linatisha kutemba usiku |
| 116. Alilemo akasokapo kughuka ulukaomano | Alikula akaondoka kwenda Mkutanoni |
| 117. Ikibufu jali nkati | Choo kilikuwa ndani |
| 118. Damas jo pachipatala | Damasi alikuwa hospitalini. |